# شرح السنة

# *Sharh-us-Sunnah*

[Ufafanuzi wa Sunnah]


*Mwandishi:*

الإمام أبو مُحَمَّد الحسن بن خلف البربهاري

**Imaam Abu Muhammad al-Hasan bin Khalaf al-Barbahaariy**

*Tarjama (na maelezo):*

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

بسم الله الرحمن الرحيم

Himdi zote anastahiki Allaah ambaye ametuongoza katika Uislamu, akatuenzi nao na akatufanya kuwa katika Ummah bora. Tunamuomba mafanikio katika yale Anayoyapenda na Kuyaridhia pamoja na kutuhifadhi kutokamana na yale Anayoyabughudhi na Kuyachukia.

1- Tambua[1] kuwa Uislamu ndio Sunnah[2] na Sunnah ndio Uislamu na kimoja katika hayo hakisimami isipokuwa kwa kingine.

2- Ni katika Sunnah kulazimiana na al-Jamaa´ah[3]. Ambaye hataki kuwa katika al-Jamaa´ah na akafarikiana nayo, basi ameivua kamba ya Uislamu katika shingo yake na atakuwa ni mpotevu mwenye kupoteza.

---

[1] ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema akifafanua maana ya neno hili ambalo limekaririwa mara nyingi katika kitabu hichi:

"Neno hili huletwa kutanabahisha umuhimu wa jambo na uwajibu wa kutanabahi nalo. Maana yake ni kwamba jifunze." (Mkanda "Sharh Nawaaqidh-il-Islaam" (01))

[2] Wingi ni Sunan. Njia, mwenendo n.k. Imaam Muhammad bin Swaalih bin ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amefafanua "Sunnah" ifuatavyo:

"Sunnah maana yake kilugha ni njia na kiistilahi ni yale aliyokuwa akifuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa saallam) na Maswahabah zake katika mambo ya ´Aqiydah au matendo." (Sharh Lum´at-il-I´tiqaad, uk. 40)

[3] Wingi ni Jamaa´aat. Kundi, Ummah n.k. ´Abdullaah bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"al-Jamaa´ah ni yale yenye kuafikiana na haki hata kama utakuwa peke yako." (al-Hawaadith al-Bid´ah, uk. 22, ya Abu Shaamah).

´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Jilazimieni na al-Jamaa´ah na jiepusheni na mfarakano. Hakika Shaytwaan yuko na aliye peke yake, ilihali yuko mbali kabisa na wale walio wawili." (Ahmad (01/18), at-Tirmidhiy (2165), an-Nasaa´iy katika "al-Kubraa" (9219) na (9226) na wengineo.)

Shaykh Swaalih Aalush-Shaykh (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"al-Jamaa´ah ni Ahl-ul-´Ilm, Ahl-ul-Hadiyth na Ahl-ul-Athar. Ameyanukuu maneno hayo al-Khatwiyb al-Baghdaadiy kwenye kitabu chake "Sharaf Asw-haab-il-Hadiyth" kwa isnadi zake mpaka kwa aliyoyasema." (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 82)

3- Msingi ambao al-Jamaa´ah imejengwa juu yake ni Maswahabah[4] wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Yule asiyechukua kutoka kwao amepotea na kuzusha. Kila Bid´ah ni upotevu na upotevu na watu wake ni Motoni[5].

4- ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Hakuna udhuru kwa yeyote katika upotevu aliyofanya huku akidhania kuwa ni uongofu, na wala kwa uongofu aliouacha huku akidhania kuwa ni upotevu. Mambo yamebainishwa, hoja zimethibiti na udhuru umekatika."[6]

---

[4] Imaam Ibn Hajar (Rahimahu Allaah) amesema:

"Swahabah ni yule ambaye amekutana na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), akamuamini na akafa hali ya kuwa ni Muislamu. Katika wao kunaingia pia yule ambaye alikaa muda mrefu na yeye na ambaye pia alikaa muda mfupi na yeye, aliyepokea kutoka kwake na ambaye hakupokea kutoka kwake, ambaye alipigana vita bega kwa bega pamoja naye na ambaye hakupigana vita bage kwa bega pamoja naye, ambaye alimuona lakini akawa hakukaa naye na yule ambaye hakumuona kwa sababu ya kizuizi, kwa mfano upofu." (al-Iswaabah (01/07))

[5] Jaabir bin ´Abdillaah (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesimulia kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Kila Bid´ah ni upotevu na kila upotevu ni Motoni." (an-Nasaa´iy katika "al-Jumu´ah (03/188) na al-Bayhaqiy katiak "al-Asmaa´ was-Swiffaat" (01/145). Ni Swahiyh kwa mujibu wa Ibn Taymiyyah katika "al-Fataawaa al-Kubraa" (03/163))

Imaam Abu Ishaaq ash-Shaatwibiy (Rahimahu Allaah) ameifafanua Hadiyth na kusema:

"Wanachuoni wameifahamu kwa njia ya iliyoenea. Hakukufanywa uvuaji wowote kabisa. Wala hakuna (Bid´ah) yoyote ilio nzuri." (Fataawaa ash-Shaatwibiy, uk. 180-181)

´Abdullaah bin ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesema:

"Kila Bid´ah ni upotevu, hata kama watu wataiona kuwa ni nzuri." (al-Bayhaqiy katika "al-Madkhal ilaa as-Sunnah" (191), Ibn Naswr katika "as-Sunnah", uk. 24, na al-Laalakaa´iy (126))

Imaam Ahmad bin Hanbal (Rahimahu Allaah) amesema:

"Tunaonelea kuwa misingi ya Sunnah ni ifuatayo: Kushikamana na yale aliyokuwemo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kuwafanya kama kiigizo na kuacha Bid´ah, kwani kila Bid´ah ni upotevu." (Usuwl-us-Sunnah, uk. 25)

Imaam Maalik bin Anas (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mwenye kuzua Bid´ah katika Uislamu na akaona kuwa ni nzuri, basi amedai kuwa Muhammad alifanya khiyana katika Ujumbe, kwa kuwa Allaah anasema: "Leo hii Nimekukamilishieni dini yenu na nimekutimizieni neema Yangu. Nimeridhia Uislamu iwe ndio dini yenu." Kile ambacho hakikuwa dini kipindi hicho leo hakiwezi kuwa dini." (al-I´tiswaam (01/49) ya ash-Shaatwibiy)

[6] al-Ibaanah al-Kubraa (162) ya Ibn Battwah al-´Ukbariy.

Hili ni kwa sababu Sunnah na al-Jamaa´ah vimetengeneza mambo ya dini yote. Yamebainishwa kwa watu na hivyo ni wajibu kwa watu kufuata.

5- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba dini ni yenye kutoka kwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) na haikuachwa kwenye akili na maoni ya wanaume. Elimu yake ni kutoka kwa Allaah na Mtume Wake. Hivyo usifuate kitu katika matamanio yako ukaja kutoka katika dini na kutoka katika Uislamu. Hakika huna hoja yoyote. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewabainishia Ummah wake Sunnah na kuwawekea nayo wazi Maswahabah zake - nao ndio al-Jamaa´ah. Hili ndio kundi kubwa[7] na kundi kubwa ni haki na watu wake. Mwenye kwenda kinyume na Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika jambo la dini, amekufuru.

6- Tambua ya kwamba watu kamwe hawakuzusha Bid´ah isipokuwa waliacha Sunnah kiasi chake. Tahadhari Muhdathaat, kwani hakika kila Muhdathah ni Bid´ah, kila Bid´ah ni upotevu na kila upotevu na watu wake ni Motoni.

7- Tahadhari na Muhdathaat ndogo ndogo, kwani hakika Bid´ah ndogo ndogo hupea mpaka zinakuwa kubwa. Kila Bid´ah iliyozushwa katika Ummah huu mwanzo wake ilikuwa ndogo na inafanana na haki. Hivyo akadanganyika yule aliyetumbukiaemo na matokeo yake hakuweza kutoka ndani yake. Ikapea na ikawa ni dini ambayo mtu anafuata. Natija yake mtu akaenda kinyume na Njia iliyonyooka na akatoka katika Uislamu.

8- Zingatia - Allaah akurehemu - kila ambaye utasikia maneno yake miongoni mwa watu wa zama zako usifanye haraka na wala usijiingize katika chochote katika hayo mpaka kwanza uulize na uchunguze: Je, Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) waliyazungumza au kuyafanya? Ukipata upokezi kutoka kwao kuhusu hayo, basi shikamana nayo. Usiyavuke na ukachagua kitu kingine ukaja kutumbukia Motoni.

[7] as-Sawaad al-A´dhwam. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ummah huu hauwezi kukusanyika katika upotevu. Mkono wa Allaah uko juu ya al-Jamaa´ah. Kwa hivyo shikamaneni na kundi kubwa na yule mwenye kuukhalifu, basi amekhalifu kwenye Moto." (Ibn Abiy ´Aaswim (80) na al-Haakim (1/115-117)).

Imaam Ibn-ul-Athiyr al-Jazariy (Rahimahu Allaah) amefasiri neno "as-Sawaad al-A´dhwam" na kusema:

"Kundi kubwa la watu ni wale waliokusanyika katika kumtii mtawala na kushikamana na mfumo uliyonyooka." (an-Nihaayah (1/822).

9- Tambua kupinda kutoka katika Njia iliyonyooka ni kwa namna mbili. Wa kwanza ni mtu ameteleza akapinda na Njia, pamoja na kuwa hakukusudia isipokuwa kheri. Kosa lake lisichukuliwe kama kiigizo, kwa sababu ni mwenye kuangamia. Mwingine, ameenda kinyume na haki na yale wachaji Allaah waliyokuwemo kabla yake. Huyo ni mpotevu na ni mwenye kuwapoteza wengine na ni shaytwaan aliyeasi katika Ummah huu. Yule mwenye kumfahamu ni lazima kwake kutahadharisha naye na kuwabainishia watu hali yake ili asije yeyote akatumbukia katika Bid´ah yake na akaangamia.

10- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba hautatimia Uislamu wa mja mpaka awe ni mwenye kufuata, mwenye kusadikisha na mwenye kujisalimisha. Yule mwenye kudai ya kwamba kuna jambo lolote katika Uislamu ambalo hawakututosha nalo Maswahabah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), amewatuhumu uongo. Hilo litatosha kuwa ni kujitenga nao na ni kuwatukana. Ni Mubtadi´[8] mpotevu na mwenye kuwapoteza wengine na mwenye kuzusha katika Uislamu yasiyokuwemo.

11- Tambua - Allaah akurehemu - hakuna kutumia kipimo katika Sunnah[9]. Hazipigiwi mfano kwa kitu na wala hazifuatwi kwa matamanio. Badala yake inatakiwa kusadikisha mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pasi na kuulizia namna na wala maelezo. Wala mtu asiseme: "Kwa nini?" au "Vipi?".

12- Falsafa, ugomvi, majadiliano na ubishi vyote ni uzushi[10]. Yanatia shaka katika moyo hata kama mwenye kujishughulisha nayo atapatia na kuzungumza kwa Sunnah.

13- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba kuchunguza kuhusu Mola ni uzushi, Bid´ah na upotevu. Hakuzungumzwi juu ya Allaah isipokuwa kwa

[8] Shaykh ´Ubayd al-Jaabiriy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Mubtadi´ ni yule mwenye kuendelea kushikamana na Bid´ah baada ya kusimamishiwa haki." (Mkanda "Jinaayat-ut-Tamayyu´ ´alaa Manhaj-is-Salafiy"")

[9] ´Allaamah Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Neno "Sunnah" lililokuja hapa makusudio ni ´Aqiydah." (Sharh-us-Sunnah, uk. 53)

[10] Imaam al-Hasan al-Baswriy (Rahimahu Allaah) alimwambia mtu mmoja ambaye alikuwa anataka kujadiliana naye:

"Ama kuhusu mimi, ninaielewa dini yangu. Lakini ikiwa wewe umepoteza dini yako, basi nenda na uitafute." (ash-Shariy´ah (241) ya al-Aajurriy)

yale aliyojisifu Mwenyewe katika Qur-aan na yale Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliyowabainishia Maswahabah zake. Hakika Yeye (Jalla Thanaa´uh) ni Mmoja:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona."[11]

14- Mola wetu ni wa Mwanzo pasi na [kuuliza] ni lini [ameanza] na ni wa Mwisho pasi na kikomo. Anayajua ya siri na yaliyofichikana na amelingana juu ya ´Arshi[12]. Elimu Yake iko kila mahali na haikosekani mahali kote.

15- Hakuna mwenye kusema juu ya Sifa za Allaah "Vipi" au "Kwa nini" isipokuwa yule mwenye shaka na Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

16- Qur-aan ni maneno ya Allaah[13], Uteremsho Wake na Nuru Yake. Haikuumbwa, kwa sababu Qur-aan inatokamana na Allaah na chenye

---

[11] 42:11

[12] Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema kumuuliza mjakazi:

"Allaah yuko wapi?" Akajibu: "Juu ya mbingu." Akamuuliza tena: "Mimi ni nani?" Akajibu: "Wewe ni Mtume wa Allaah." Ndipo akasema: "Mwache huru, kwani hakika ni muumini." (Muslim (537))

Imaam Mujaahid bin Jabr al-Makkiy (Rahimahu Allaah) - mwanafunzi wa Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amefafanua neno "Mwingi wa Rahmah *Istawaa´* juu ya ´Arshi" (20:05):

"Istawaa´ maana yake ni kulingana juu." (al-Bukhaariy (1554))

Imaam Ibn Jariyr at-Twabariy (Rahimahu Allaah) pia amefafanua maana ya neno liliyoko juu na kusema:

"Maana yake ni kulingana juu na kung´atika." (Jaami´-ul-Bayaan (01/192))

Imaam al-Hasan al-Baghawiy (Rahimahu Allaa) amepokea ya kwamba Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amefasiri maneno ya Allaah yaliyoko juu ifuatavyo:

"Yuko juu ya mbingu." (Ma´aalim-ut-Tanziyl (01/59))

[13] Imaam Sufyaan bin ´Uyaynah (Rahimahu Allaah) amefafanua maneno ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) "Ni Vyake Pekee uumbaji na amri" (07:54):

"Uumbaji ni uumbaji wa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) na amri ni Qur-aan." (ash-Shariy´ah (69) ya al-Aajurriy)

Imaam Muhammad bin Idriys ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

kutokamana na Allaah hakikuumbwa. Hivyo ndivyo alivyosema Maalik bin Anas[14], Ahmad bin Hanbal[15] na Fuqahaa´ kabla yao na baada yao. Na kujadiliana juu yake ni kufuru.

17- Kuamini Muonekano siku ya Qiyaamah[16]. Watamuona Allaah (´Azza wa Jall) kwa macho yaliyo vichwani mwao[17] na yeye atawafanyia hesabu pasi na pazia wala mkalimani.

18- Kuamini Mizani siku ya Qiyaamah ambapo kheri na shari vitapimwa. [Mizani ina] vitanga viwili na ulimi.

19- Kuamini adhabu ya kaburi[18] pamoja na Munkar na Nakiyr[19].

---

"Qur-aan ni maneno ya Allaah na haikuumbwa. Mwenye kusema kuwa imeumbwa ni kafiri." (al-Ibaanah (02/775) ya Ibn Battwah).

[14] Imaam Maalik bin Anas (Rahimahu Allaah) amesema:

"Qur-aan ni maneno ya Allaah na haikuumbwa." (Sharh Usuwl I´tiqaad Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa´ah (414) ya al-Laalakaa´iy).

Kadhalika Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu yule mwenye kusema kuwa Qur-aan imeumbwa:

"Anatakiwa kuadhibiwa kwa kipigo na kutiwa jela mpaka afe." (ash-Shaariy´ah (79) ya al-Aajurriy)

[15] Imaam Ahmad bin Hanbal (Rahimahu Allaah) alisema pindi alipoulizwa juu ya mwenye kusema kuwa Qur-aan imeumbwa:

"Ni kafiri." (Sharh usuwl I´tiqaad Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa´ah (449) ya al-Laalakaa´iy)

[16] Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Hakika mtamuona Mola wenu kama jinsi mnavyouona mwezi huu - hamtosongamana katika kumuona." (al-Bukhaariy (50) na (6777) na Muslim (08))

[17] ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Kwa nini amesema "siku ya Qiyaamah"? Kwa sababu (Jall wa ´Alaa) haonekani hapa duniani.

Kwa macho yaliyo vichwani mwao huku ni kukanusha Ta´wiyl za wale wanaosema:

"... watamuona."

maana yake ni kwa nyoyo zao na si kwa macho yao." (Sharh-us-Sunnah, uk. 75)

[18] ´Abdullaah bin ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesimulia: "Mtume wa Allaah alipita karibu na makaburi mawili na akasema:

20- Kuamini Hodhi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kila Mtume ana hodhi isipokuwa tu Swaalih (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni maziwa ya ngamia wake[20].

21- Kuamini uombezi wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[21] kwa watenda madhambi na waliokosea siku ya Qiyaamah na katika

---

"Hakika hawa wawili wanaadhibiwa na hawaadhibiwi kwa kitu kikubwa." Halafu akasema: "Ama kuhusu mmoja wao alikuwa hajilindi na cheche za mikojo na mwengine alikuwa akieneza uvumi."" (al-Bukhaariy (218) na Muslim (292))

Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Hakika adhabu ndani ya kaburi ni haki, kuhojiwa ndani ya kaburi ni haki, Kusimamishwa [siku ya Qiyaamah] ni haki, Hesabu ni haki, Pepo na Moto ni haki na kila kilichoelezwa katika Sunnah na kutajwa na wanachuoni, na maswahiba zao katika miji ya Kiislamu, ni haki." (Manaaqib ash-Shaafi´iy (01/415) ya al-Bayhaqiy)

Imaam Abul-Hasan al-Ash´ariy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kuna Maafikiano juu ya kwamba adhabu ndani ya kaburi ni haki na kwamba watu watajaribiwa na kuhojiwa kwenye makaburi yao." (Risaalah ilaa Ahl-ith-Thaghr, uk. 279)

[19] Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) amepokea ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Pindi mmoja wenu anapowekwa kwenye kaburi lake, basi hujiwa na Malaika wawili weusi walio na macho ya kijani. Mmoja anaitwa al-Munkar na mwengine anaitwa an-Nakiyr. Wanamwambia: "Ulikuwa unasemaje juu ya mtu huyu?" Atasema yale aliyokuwa akisema, nayo: "Ni mja na Mtume wa Allaah. Ninashuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake." Ndipo watasema: "Tulijua kwamba ulikuwa ukisema hivo." Baada ya hapo kaburi lake lipanuliwe dhiraa sabini upana na urefu." (at-Tirmidhiy (1077) na Ibn Hibbaan (780). Ni nzuri kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh al-Jaami´ as-Swaghiyr" (01/724))

[20] ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Uvuaji (*Istithnaa´*) hii haikuthibiti kutokana na ninavyojua. Sahihi ni kuwa Mitume wote wana hodhi. Hivyo ndivyo ilivyotajwa katika Hadiyth." (Sharh-us-Sunnah, uk. 81)

Samurah (Radhiya Allaahu ´anh) amepokea kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Kila Mtume yuko na hodhi na watajifakhari ni nani ambaye atapata watu wengi. Ninamuomba Allaah nipate watu wengi kuliko wao." (al-Bukhaariy katika "at-Taariykh al-Kabiyr" (01/01/44), Ibn Abiy ´Aaswim (734) na wengineo. Ni Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwilaal-ul-Jannah", uk. 336, na "Silsilah al-Ahaadiyth as-Swahiyhah" (1589))

[21] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Atakuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku ya Qiyaamah na nyombezi tatu. Ama uombezi wa kwanza atawaombea waliosimamishwa na kusubiri wahukumiwe baada ya Aadam, Nuuh, Ibraahiym,

Njia[22]. Atawatoa kutoka kwenye rindi la Moto. Kila Mtume ana uombezi na kadhalika wakweli, mashahidi na waja wema. Baada ya hapo Allaah ataonyesha fadhila nyingi kwa yule Anayemtaka na baada ya kuwa wameungua na wamekuwa mkaa, watatoka Motoni.

22- Kuamini Njia ilioko juu ya Moto. Njia itamkaba yule Allaah anamtaka, itamwacha yule Allaah anamtaka na ataanguka ndani ya Moto yule Allaah anamtaka. Watakuwa na mwanga kutegemea na imani zao.

23- Kuamini Mitume na Malaika.

24- Kuamini kuwa Pepo na Moto vyote ni haki. Vyote viwili vimeumbwa. Pepo iko kwenye mbingu ya saba na sakafu yake ni ´Arshi, wakati Moto uko chini kabisa ya ardhi ya saba. Vyote viwili vimeumbwa. Allaah (Ta´ala) anajua idadi ya watu wa Peponi na ni nani atayeingia na idadi ya watu wa Motoni na wataouingia. Vitu viwili hivyo havitotoweka kamwe na vitabaki kwa kubakia kwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) kwa muda wa kudumu milele na milele.

25- Aadam (´alayhis-Salaam) alikuwa katika Pepo ya milele, iliyoumbwa. Baada ya hapo akatolewa baada ya kumuasi Allaah (´Azza wa Jall).

---

Muusa na ´Iysa bin Maryam kutoa udhuru wa kuombea, mpaka itaishia kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ama uombezi wa pili atawaombea watu wa Peponi waingie Peponi – na nyombezi hizi mbili ni maalum kwake. Ama uombezi wa tatu atawaombea wale waliostahiki kuingia Motoni. Na uombezi huu ni kwake na kwa Mitume wengine, wakweli na wengineo. Atawaombea wale waliostahiki kuingia Motoni wasiingizwe na awaombee wale walioingia watolewe humo. Allaah (Ta´ala) Atawatoa ndani ya Moto watu si kwa sababu ya uombezi, bali ni kwa sababu ya fadhila na huruma Wake. Kutabaki Peponi nafasi baada ya watu walioingia na Allaah Ataumba watu maalum kwa ajili yake kisha Awaingize Peponi. Hatua hizi mbali mbali zinazokujakuhusu Nyumba ya ´Aakhirah, hesabu na thawabu, Pepo na Moto." (al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 100-101)

[22] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Katika kiwanja cha Qiyaamah kutakuwa hodhi iliyotajwa ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Maji yake ni meupe kuliko maziwa na matamu kuliko asali. Vikombe vyake ni wingi wa idadi ya nyota mbinguni na urefu na upana wake ni sawa na mwendo wa mwezi. Anayekunywa humo mara moja, hatopata kiu baada yake kamwe. Njia imewekwa juu ya Jahannam na ni daraja iliyo baina ya Pepo na Moto. Watu watapita juu yake kadiri ya matendo yao. Kuna ambao watapita kama kufumba na kufumbua, wengine kama umeme, wengine kama upepo, wengine kama mpanda farasi, wengine kama mwenye kusafiri kwa ngamia, wengine kama mkimbiaji, wengine kama watembeaji, wengine kama mtambaaji na wengine watashikwa na kutupwa Motoni. Yule atakayevuka Njia ataingia Peponi. Watapoivuka watasimama kwenye daraja baina ya Pepo na Moto na kulipizana kisasi wao kwa wao. Baada ya kusafishwa, watapewa idhini ya kuingia Peponi. Mtu wa kwanza ambaye atafunguliwa mlango wa Pepo ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na watu wa kwanza ambao wataingia Peponi ni Ummah wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)." (al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 99-100)

26- Kuamini al-Masiyh ad-Dajjaal[23].

27- Kuamini kuwa ´Iysaa bin Maryam (´alayhis-Salaam) atateremka. Atashuka na kumuua ad-Dajjaal. Hali kadhalika ataoa na kuswali nyuma ya Imaam kutoka katika kizazi cha Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Atakufa na waislamu watamzika.

28- Kuamini kuwa imani ni maneno na matendo, matendo na maneno na nia na lengo[24]. Inazidi na kupungua. Inazidi vile Allaah anavyotaka na inashuka mpaka hakubaki kitu chochote[25].

---

[23] Anas bin Maalik (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliyesema:

"Allaah hakutuma Mtume yeyote isipokuwa aliwatahadharisha watu wake na al-Masiyd ad-Dajjaal. Hakika ana jicho moja na Mola wenu hana jicho moja. Katikati ya jicho lake kutakuwa "Kaafir"." (al-Bukhaariy (7408) na (7131) na Muslim (2933)).

Imaam Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Hadiyth kuhusiana na suala hili zimepokelewa na Maswahabah wengi mno [Mutawaatir], jambo ambalo limethibitishwa na wanachuoni wengi bingwa." (Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah, uk. 59).

[24] Imaam Ibn Qudaamah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Imani ni kutamka kwa ulimi, matendo ya viungo na kuamini moyoni. Inazidi kwa utiifu na inapungua kwa maasi. Allaah (Ta´ala) amesema: "Na hawakuamrishwa chochote isipokuwa wamwabudu Allaah wakiwa wenye kumtakasia Yeye dini, kwa imani iliokuwa safi, na wasimamishe swalah na watoe zakaah - na hiyo ndiyo dini iliyosimama imara." (98:05) Kafanya kumuabudu Allaah (Ta´ala), kuutakasa moyo, kusimamisha swalah na kutoa zakaah, yote hayo yanaingia katika dini. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema: "Imani ni tanzu sabini na kitu. Ilio juu kabisa ni kusema "nashuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah... " na ilio chini ni kuondoa chenye kudhuru njiani." al-Bukhaariy (09) na Muslim (35). Amefanya kutamka na kutenda vyote vinaingia katika katika imani." (Lum´at-il-I´tiqaad, uk. 15)

[25] al-Humaydiy amesema:

"Nilimsikia Sufyaan bin ´Uyaynah akisema: "Imani ni maneno na matendo. Inazidi na kushuka." Ndipo ndugu yake mdogo Ibraahiym bin ´Uyaynah akasema: "Ee Abu Muhammad! Unasema kuwa inashuka?" Akasema: "Kaa kimya we mtoto! Inaweza kushuka mpaka kusibaki kitu." (´Aqiydat-us-Salaf wa Asw-haab-il-Hadiyth (95) ya as-Swaabuuniy)

Imaam al-Aajurriy (Rahimahu Allaah) amepokea ya kwamba kulisemwa kuambiwa Imaam Sufyaan bin ´Uyaynah: "Je, imani inapanda na kushuka?" Akajibu:

"Hamsomi maneno ya Allaah: "Ili wazidi imani juu ya imani zao." (48:04)? Kukasemwa: "Inashuka?" Ndipo akajibu: "Hakuna kitu kinachozidi isipokuwa kadhalika kinashuka." (120)

29- Mbora wa Ummah huu baada ya Mitume wake kufa ni: Abu Bakr, ´Umar na ´Uthmaan. Namna hii ndivyo ilivyopokelewa kwetu kutoka kwa Ibn ´Umar, ambaye amesema:

"Tulikuwa tukisema na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yuko kati yetu: "Hakika mtu bora baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Abu Bakr, ´Umar na ´Uthmaan. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akiyasikia hayo na wala hayapingi.""[26]

Halafu watu bora baada ya watu hawa ni: ´Aliy, Twalhah, az-Zubayr, Sa´d bin Abiy Waqqaas, Sa´iyd bin Zayd, ´Abdur-Rahmaah bin ´Awf na Abu ´Ubaydah bin al-Jarraah. Wote hawa walikuwa wanastahiki ukhalifah. Kisha watu bora baada ya hawa ni: Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), karne ya kwanza aliyotumwa kwao: Wahajiri wa kwanza na Wanusuraji walioswali katika Qiblah zote mbili[27]. Halafu watu bora baada ya hawa ni: wale waliosuhubiana na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku moja, mwezi mmoja, mwaka mmoja au chini au zaidi ya hapo. Watakiwa rahmah, zitaje fadhila zao, jiepushe na kutaja kasoro zao na hatumtaji yeyote katika wao isipokuwa kwa njia ya kheri. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Wanapotajwa Maswahabah zangu basi nyamazeni."[28]

Sufyaan bin ´Uyaynah amesema:

"Mwenye kutamka neno japo moja tu kwa kuwasema vibaya Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi ni mtu anayefuata matamanio."

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Maswahabah zangu ni kama nyota yeyote utakayemfuata, basi utaongoka."[29]

---

[26] al-Bukhaariy katika "Fadhwaa-il-us-Swahaabah" (07/12) na Ahmad katika "Fadhwaa-il-us-Swahaabah" (53-59).

[27] Quds na Ka´bah.

[28] at-Twabaraaniy katika "al-Kabiyr" (10/243-244) na Abu Nu´aym (04/108).

[29] Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

30- Inatakiwa kuwasikiliza na kuwatii viongozi katika yale Allaah anayoyapenda na kuyaridhia. Mwenye kutawalia ukhalifa baada ya watu kuafikiana juu yake na kuridhika naye, basi huyo ni kiongozi wa waumini.

31- Si halali kwa yeyote kulala japo usiku mmoja na hali ya kuwa haonelei kuwa ana kiongozi juu yake, ni mamoja awe ni mwema au mtenda maovu.

32- Hajj na vita vitaendelea kuwepo pamoja na kiongozi. Swalah ya Ijumaa nyuma yao inajuzu. Ataswali Rakaa´ sita baada ya Ijumaa, atazipambanua baina ya kila Rakaa´ mbili. Haya ni maoni ya Ahmad bin Hanbal[30].

33- Ukhalifah utaendelea kuwa haki ya Quraysh mpaka pale ataposhuka ´Iysaa bin Maryam (´alayhis-Salaam).

34- Atayefanya uasi dhidi ya kiongozi mmoja wapo wa waislamu ni Khaarijiy[31]. Atakuwa ameugawa umoja wa waislamu, ameenda kinyume na mapokezi na kifo chake ni kifo cha Jaahiliyyah[32].

---

"Hadiyth hii ni dhaifu. al-Bazzaar amesema: "Maneno haya hayakuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)." Ibn Hazm amesema: "Ni ya uongo, uzushi na batili." Ibn Kathiyr amesema: "Hakuna yeyote katika watunzi wa vile vitabu sita aliyepokea Hadiyth hii na ni dhaifu." Kadhalika al-´Iraaqiy, Ibn Hajar na al-Albaaniy wameidhoofisha. Tazama "al-Madkhal", uk. 162-164 ya al-Bayhaqiy, "Tuhfat-ut-Twaalib", uk. 165-166 ya Ibn Kathiyr, "al-Mu´tabar", uk. 82-85 ya az-Zaraakshiy, "Takhriyj Ahaadiyth-il-Minhaaj", uk. 81-86 ya al-´Iraaqiy, "as-Silsilah adh-Dhwaa´iyfah" (58-62) ya al-Albaaniy." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (29))

[30] Tazama "Twabaqaat-ul-Hanaabilah" (01/42, 241, 294, 311, 329 na 342).

[31] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema pindi alipokuwa akifafanua maneno ya Imaam at-Twahaawiy kuhusu kutowafanyia uasi watawala yafuatayo:

"Hii ndio ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Hawaonelei kufanya uasi kwa watawala kwa sababu ya maasi hata kama watafanya unyanyasaji na kudhulumu. Vilevile hatujivui kutoka katika utiifu wala [hatuonelei] kuwachochea watu kuwafanyia uasi. Tunawaombea kunyooka na hatuwaombei du´aa dhidi yao. Hii ndio ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah tofauti na Ahl-ul-Bid´ah miongoni mwa Khawaarij na Mu´tazilah na Raafidhwah. Hii ndio sababu ya mwandishi (Rahimahu Allaah) na wengine kuingiza haya katika vitabu vya ´Aqiydah.

Khawaarij wanaona kusihi kufanya uasi kwa mtawala kwa sababu ya maasi. Mtawala akifanya maasi wanaona kuwa ni kafiri na inafaa kumuua na kumg´oa katika uongozi. Haya ni madhehebu batili.

Vilevile Mu´tazilah wanaona kuwa mtawala akitenda dhambi kubwa kama kunywa pombe basi ni wajibu kumfanyia uasi kwa sababu ametoka katika imani na kuingia katika kufuru na kumdumisha Motoni.

Kadhalika Raafidhwah wanaona kusihi kumfanyia uasi mtawala kwa sababu ya maasi kwa kuwa wanaona kuwa uongozi wake ni batili. Bali wao hawaonelei kuwepo kwa uongozi isipokuwa yule kiongozi ambaye amekingwa na kukosea. Ama viongozi wengine uongozi wao ni batili. Maimamu waliokingwa na kukosea

35- Si halali kumpiga vita mtawala na kufanya uasi dhidi yao, hata kama watafanya dhuluma. Haya yamejengwa juu ya maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipomwambia Abu Dharr al-Ghiffaariy:

"Kuwa na subira, hata kama atakuwa ni mja wa kihabeshi."[33]

Vilevile aliwaambia Wanusuraji:

"Kuweni na subira mpaka mtapokutana na mimi kwenye Hodhi."[34]

Sio katika Sunnah kumpiga vita mtawala. Hakika ni jambo ndani yake kuna ufisadi katika dini na dunia.

36- Ni halali kuwapiga vita Khawaarij endapo watawavamia waislamu maisha yao, mali zao na familia zao. Hata hivyo si halali ikiwa watakimbia kuwatafuta. Mtu asiwaue wajeruhi wao, asichukue ngawira zao, asiwaue wafungwa wao na asiwafuate wale wenye kukimbia.

37- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba haifai kumtii yeyote katika kumuasi Allaah (´Azza wa Jall)[35].

---

ni wale kumi na mbili ambao ameteuliwa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) - kama wanavyodai." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (02/546-548)

Sa´iyd bin Jamhaan amesema:

"Nilifika kwa ´Abdullaah bin Abiy Awfaa ambaye alikuwa ni kipofu. Nikamtolea salaam akanambia: "Wewe ni nani?" Nikasema: "Mimi ni Sa´iyd bin Jamhaan." Akasema: "Baba yako alifanya nini?" Nikajibu: "Azaariqah [kundi katika Khawaarij] walimuua." Ndipo akasema: "Allaah awalaani Azaariqah. Allaah awalaani Azaariqah. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitueleza kwamba ni mijibwa ya Motoni." Nikasema: "Inahusu Azaariqah peke yao au ni Khawaarij wote?" Akasema: "Hapana, ni Khawaarij wote." (Ahmad. al-Albaaniy ameifanya kuwa ni nzuri katika "Dhwilaal-ul-Jannah", uk. 523)

[32] Imaam Ibn Kathiyr (Rahimahu Allaah) amefasiri neno "Jaahiliyyah" ifuatavyo:

"Ni hali walokuwa nayo waarabu kabla ya kuja Uislamu na ambayo ilikuwa na ujinga juu ya Allaah, Mtume Wake na Shari´ah za Kiislamu. Kadhalika ina maana ya kujifakhari kwa kabila na vilevile kujiona, jeuri n.k." (an-Nihaayah (01/323)).

[33] Muslim (1837), Ahmad (03/171) na Ibn Maajah (2862).

[34] al-Bukhaariy (07/117) pamoja na "Fath-ul-Baariy", Muslim (1845) na Ahmad (03/57).

[35] ´Abdullaah bin ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ni juu ya kila Muislamu kusikiliza na kutii katika yale anayoyapenda na kuyachukia maadamu hakuamrishwa maasi. Endapo ataamrishwa maasi, hakuna usikivu wala utiifu." (Muslim (1839))

38- Usimshuhudilie Muislamu yeyote kwa sababu ya kitendo chake cha kheri au cha shari, kwa sababu hujui ni hali gani aliyohitimisha nayo wakati wa kufa. Badala yake unatakiwa kutarajia juu yake rehema za Allaah na kukhofia kwake kutokana na madhambi yake. Vilevile hujui alichojutia mbele ya Allaah kabla ya kufa na alichofanya Allaah kitokee katika kipindi hicho ikiwa atakufa kama Muislamu. Hivyo tarajia juu yake rehema za Allaah na ukhofie kwake kutokana na madhambi yake.

39- Hakuna dhambi yoyote ambayo mja hawezi kutubia kwayo.

40- Kupigwa mawe ni haki[36].

41- Ni Sunnah mtu kupangusa juu ya khufuu[37].

---

[36] ´Ubaadah bin as-Swaamit (Radhiya Allaahu ´anh) amepokea kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Pokea kutoka kwangu, pokea kutoka kwangu! Allaah amewapa wanawake njia; mwanaume ambaye hajaoa akizini na mwanamke ambaye hajaolewa, adhabu ni bakora mia na kutimuliwa mwaka mmoja. Mwanaume ambaye kishaoa akizini na mwanamke ambaye kishaolewa wanatakiwa kupigwa bakora mia na baada ya hapo kupigwa mawe mpaka wafe." (Muslim (1690))

Imaam an-Nawawiy (Rahimahu Allaah) amefafanua Hadiyth iliyopo juu na kusema:

"Mpangilio huu sio sharti. Adhabu ya ambaye hajaingia katika ndoa ni ile ile sawa ikiwa atazini na ambaye hajaingia katika ndoa au kishaingia katika ndoa. Adhabu ya ambaye kishaingia katika ndoa ni kupigwa mawe sawa awe alifanya na ambaye kishaoa/olewa au hajaoa/olewa. Tambua ya kwamba mtu ambaye hajaingia katika ndoa ni mwanaume au mwanamke ambaye hajafanya jimaa ndani ya ndoa sahihi; aliye huru, ambaye kishabeleghe na akili zake. Mambo ni namna hiyo ikiwa alifanya jimaa ndani ya ndoa iliyo na mashaka, ndoa ambayo si sahihi au mfano wa hayo na yasiyokuwa hayo. Kuhusu mtu ambaye kishaingia katika ndoa ni yule ambaye alifanya jimaa ndani ya ndoa sahihi; kishabaleghe, mwenye akili zake na aliye huru. Adhabu hiyo inamuhusu mwanaume na mwanamke - na Allaah ndiye anajua zaidi." Sharh Swahiyh Muslim (11/157)

[37] Kuhusu kupangusa juu ya khufuu wakati wa kutawadha imeshurutishwa kwa mwenye kufanya hivo pindi alipozivaa alikuwa yuko na wudhuu´. al-Mughiyrah bin Shu´bah (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Siku moja wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anatawadha, nikakimbia ili nimvue soksi zake za ngozi (khuff). Ndipo akasema: "Ziache, hakika mimi nilizivaa nikiwa na twahara." Kisha baada ya hapo akapangusa juu yake." (al-Bukhaariy (206) na Muslim (274))

Shurayh bin Haaniy amesema:

"Nilienda kwa ´Aaishah kumuuliza kuhusu kufuta juu ya Khufuu. Akasema: "Muulize Ibn Abiy Twaalib, kwani yeye alikuwa akisafiri na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)." Tukamuuliza akasema: " "Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amefanya mchana mmoja na usiku wake kwa mkazi na michana mitatu na nyusiku zake kwa msafiri."" (Muslim (276))

Shaykh Ibn ´Uthyamiyn (Rahimahu Allaah) aliulizwa juu ya maoni ya baadhi ya wanachuoni, nayo ni kwamba wanasema kuwa inafaa kupangusa juu ya soksi aina zote. Akajibu:

42- Ni Sunnah kufupisha swalah wakati wa safari.

43- Kuhusiana na kufunga wakati wa safari, mwenye kutaka atafunga na asiyetaka ataacha kufunga.

44- Haina neno kuswali hali ya kuwa mtu amevaa suruwali [pana].

45- Unafiki[38] ni kule mtu kudhihirisha Uislamu na kuficha ukafiri.

46- Tambua kuwa dunia ni ulimwengu wa imani na Uislamu[39].

47- Kati ya Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuna waumini inapokuja katika hukumu zao, mirathi yao, vichinjwa vyao pamoja na kuwaswalia.

48- Hatumshuhudilii yeyote kuwa na imani kamilifu mpaka atekeleze Shari´ah zote za Kiislamu. Endapo atapuuzia kitu katika hayo, anazingatiwa

---

"Maoni haya yenye kusema kwamba inajuzu kwa mtu kupangusa juu ya soksi aina zote ndio maoni sahihi. Hili ni kwa sababu maandiko yanayohusiana na kupangusa juu ya khufuu hayakufungamana na yale ambayo Shari´ah imeyataja bila ya kufungamanisha haifai kufungamanisha na kuweka masharti." (Majmuu´ Fataawaa ash-Shaykh Ibn ´Uthaymiyn (07/158))

[38] Nifaaq. Imaam ´Abdur-Rahmaan bin Naaswir as-Sa´diy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Unafiki maana yake ni kuonesha kheri na kuficha shari. Umegawanyika aina mbili:

1- Unafiki mkubwa wenye kuhusiana na imani. Aliye na unafiki aina hii atadumishwa Motoni milele. Mfano wake ni kama yale aliyoelezea Allaah kuhusu wanafiki pale aliposema:

"Miongoni mwa watu wako wasemao: "Tumemuamini Allaah na siku ya Mwisho" hali ya kuwa si wenye kuamini."" (02:08)

Hawa wanaficha ukafiri na wanaonesha imani.

2- Unafiki mdogo wenye kuhusiana na matendo. Mfano wake ni kama yale aliyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Alama za mnafiki ni tatu; anapozungumza husema uongo, anapoahidi hatimizi na anapoaminiwa anasaliti." (al-Bukhaariy (33) na Muslim (59)).

Kufuru na unafiki mkubwa haunufaishi imani na matendo. Kuhusu kufuru na unafiki mdogo, unaweza kukusanyika sehemu moja na imani. Katika hali hii mja anakuwa na kheri na shari na anastahiki thawabu na adhabu vyote viwili." (Ahamm-ul-Muhimmaat, swali la 16)

[39] Shaykh Swaalih as-Suhaymiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Anachokusudia hapa mtunzi wa kitabu ni kwamba dunia ni ulimwengu wa kuamini na kufanya ´amali tofauti na Aakhirah." (Mkanda wa taaliki yake ya Sharh-us-Sunnah)

kuwa na imani pungufu mpaka atubu. Tambua kuwa imani yake iko kwa Allaah (Ta´ala), sawa iwe ni imani kamilifu au pungufu, isipokuwa akidhihirisha kwako kupuuzia Shari´ah za Kiislamu.

49- Ni Sunnah kuwaswalia waislamu wenye kufa; waliopigwa mawe, wazinifu wanaume na wanawake, wenye kujiua na waislamu wengine. Hali kadhalika walevi na wengineo. Ni Sunnah kuwaswalia.

50- Hakuna Muislamu yeyote anayetoka katika Uislamu mpaka arudishe *Aayah* kutoka katika Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jall) au kitu kutoka katika mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), akachinja kwa ajili ya mwengine asiyekuwa Allaah au akaswali kwa ajili ya asiyekuwa Allaah. Atapofanya kitu katika hayo, basi itakuwajibikia kumtoa katika Uislamu. Asipofanya kitu katika hayo, basi ni muumini Muislamu kwa jina, na si kwa uhakika.

51- Mapokezi yote utayosikia ambayo hayakufikiwa na akili yako, kwa mfano maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Nyoyo za waja ziko baina ya Vidole viwili katika Vidole vya Allaah (´Azza wa Jall)."[40]

"Hakika Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) hushuka katika mbingu[41] ya dunia."[42]

"Anashuka siku ya ´Arafah."[43]

---

[40] Muslim (2654) na Ahmad (02/168).

[41] Imaam Fudhwayl bin ´Iiyaadhw (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mtu katika Jahmiyyah akikwambia: "Mimi simuamini Mola anayeshuka chini kutoka sehemu Yake" wewe mwambie: "Mimi namuamini Mola anayefanya kile Anachokitaka." (´Aqiydat-us-Salaf wa Asw-haab-il-Hadiyth (71) ya as-Swaabuuniy)

Imaam as-Swaabuuniy (Rahimahu Allaah) amesema kuhusiana na Hadiyth hii: "Allaah (Ta´ala) hushuka katika mbingu ya dunia na kusema: "Mimi ni mfalme, Mimi ni mfalme (mara tatu)! Nani mwenye kuniomba, Nimpe? Nani mwenye kuniomba, Nimuitikie? Nani mwenye kuniomba msamaha, Nimsamehe?" mpaka kunapopambazuka.":

"Nilimsikia mwalimu wetu Abu Mansuur akisema baada ya kunukuu Hadiyth hii, kwamba kuna mtu alimuuliza Abu Haniyfah juu yake. Akajibu: "Anashuka, lakini hatujui namna."" (´Aqiydat-us-Salaf wa Asw-haab-il-Hadiyth (62-63))

[42] al-Bukhaariy (03/29) pamoja na "Fath-ul-Baariy" na Muslim (758).

[43] Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Hakutoachwa kutupwa ndani ya Moto [watu na mawe] mpaka (Jalla Thanaa´uh) aweke Mguu Wake juu yake."[44]

Maneno ya Allaah (Ta´ala) kumwambia mja:

"Ukija Kwangu kwa kutembea, basi Mimi nitakukimbilia."[45]

"Hakika Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) hushuka siku ya ´Arafah."

"Hakika Allaah alimuumba Aadam kwa sura Yake."[46]

"Nilimuona Mola Wangu katika sura nzuri.",[47]

na mfano wa Hadiyth kama hizi, ni lazima kwako kujisalimisha, kuthibitisha na kutojiingiza katika namna yake na kuridhika na kutosheka na hilo[48]. Usifasiri kitu katika hayo kwa matamanio yako. Hakika kuamini haya ni jambo la wajibu. Yeyote atayefasiri kitu katika haya kwa matamanio yake au akarudisha kitu katika haya, basi huyo ni Jahmiy[49].

---

"Mlolongo wa wapokezi zake ni dhaifu kama ilivyotajwa katika "as-Silsilah adh-Dhwaa´iyfah" (02/125-126)." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (51))

[44] al-Bukhaariy (7384) na Muslim (2848).

[45] al-Bukhaariy (13/384) pamoja na "Fath-ul-Baariy" na Muslim (2657).

[46] al-Bukhaariy (11/03) pamoja na "Fath-ul-Baariy"

[47] Ahmad (05/243).

[48] Imaam as-Swaabuuniy (Rahimahu Allaah) amepokea kwamba Imaam ´Abdullaah bin al-Mubaarak (Rahimahu Allaah) amesema:

"Pindi Hadiyth ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) inapokujia, basi jisalimishe nayo hali ya kunyenyekea." (´Aqiydat-us-Salaf wa Asw-haab-il-Hadiyth (41)).

[49] Wingi ni Jahmiyyah. ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Jahmiyyah! Unajua nini kuhusu Jahmiyyah? Jahmiyyah ni unasibisho wa Jahm bin Swafwaan, ambaye ni mwanafunzi wa al-Ja´d bin Dirham. al-Ja´d bin Dirham alikuwa ni mwanafunzi wa Twaaluut na Twaaluut alikuwa ni mwanafunzi wa myahudi Lubayd bin al-A´swam - ni wanafunzi wa myahudi!" (Lamhah ´an al-Firaq adh-Dhwalaal, uk. 46).

Imaam Ibn ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu Jahmiyyah:

"Wanakanusha sifa za Allaah (´Azza wa Jall) na wale waliopindukia wanakanusha kabisa majina yote na kusema: "Haijuzu kumthibitishia Allaah jina wala sifa yoyote. Ukimthibitishia Allaah jina, basi umemfananisha na walio na majina. Na endapo utamthibitishia Allaah sifa, basi umemfananisha na walio

52- Mwenye kudai kuwa anamuona Mola Wake katika dunia hii, huyo hamwamini Mola Wake (´Azza wa Jall).

53- Kumfikiria Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) ni Bid´ah, kutokana na maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Fikirieni uumbaji na wala msimfikirie Allaah."[50]

kwa sababu kumfikiria Mola kunafanya mashaka kupenyeza ndani ya moyo.

54- Tambua ya kwamba wanyama wa ardhini, wanyama pori na wanyama wote wanaotambaa kama vile chungu, sisimizi na nzi, wameamrishwa. Hawafanyi kitendo chochote isipokuwa kwa idhini ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

55- Kuamini kuwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) tokea mwanzo aliyajua yote yaliyokuwepo na ambayo hayakuwepo na yaliyoko. Hakika Allaah ameyadhibiti na kuyahesabu kwelikweli. Mwenye kusema: "Hayajui yaliyokuwepo na yatayokuwepo", hamwamini Allaah, Mtukufu[51]."

---

na sifa. Kwa hivyo haifai kuthibitisha jina wala sifa yoyote! Yale majina ambayo Allaah amejithibitishia Mwenyewe ni *Majaaz*, na sio majina kihakika." (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah (02/62))

[50] Abush-Shaykh katika "al-´Adhamah (05) na Abul-Qaasim al-Aswbahaaniy katika "at-Targhiyb" (668-670).

[51] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Qadariyyah wamegawanyika sehemu mbili:

1- Qadariyyah waliyopindukia.

2- Qadariyyah walio kati kwa kati.

Qadariyyah waliyopindukia wamepinga daraja mbili za mwanzo ambayo ni kule kuyajua kwake mambo na kule kuyaandika.

Qadariyyah walio kati kwa kati wamepinga ujumla wa daraja mbili za mwisho. Wameamini elimu na uandishi wa Allaah, kwa msemo mwingine wamekiri hilo na wakasadikisha daraja mbili za mwanzo. Lakini pamoja na hivyo wamepinga ujumla wa daraja mbili za mwisho kama itakavyokuja huko mbele.

Qadariyyah waliyopindukia waliotangulia, kama mfano wa Ma´bad al-Juhaniy, ambaye Ibn ´Umar aliulizwa juu ya maneno yake, ´Amr bin ´Ubayd, wanapinga elimu ya Allaah iliyotangulia na ilioko huko mbele. Watu hawa wanadai vilevile kuwa Allaah anaamrisha na kukataza mambo lakini wakati huo huo hajui ni nani atakayemtii na atakayemuasi. Badala yake anasema kuwa mambo yako bure tu. Msemo huu ndio wa kwanza uliozushwa katika Uislamu baada ya kuisha karne za Makhaliyfah waongofu. Mtu wa kwanza aliyeleta hilo Basrah ilikuwa ni Ma´bad al-Juhaniy na mtu anayeitwa Ghaylaan ad-Dimashqiy akachukua

56- Hakuna ndoa isipokuwa kwa kuwepo walii, mashahidi wawili waadilifu na mahari, sawa yawe madogo au makubwa. Asiyekuwa na walii basi mtawala ndiye anakuwa walii wake.

57- Mwanaume anapomtaliki mwanamke mara tatu, basi anakuwa haramu kwake na hawi halali kwake mpaka aolewe na mume mwingine.

58- Si halali damu ya Muislamu ambaye anashuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni mja na Mtume wa Allaah isipokuwa kwa moja katika mambo matatu: mwenye kuzini baada ya kuingia katika ndoa, mwenye kuritadi baada ya kuamini au mwenye kuua nafsi ya muumini pasi na haki. Anapaswa kuuawa kwa ajili ya haya. Mbali na mambo haya, damu ya Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni haramu milele, mpaka Qiyaamah kisimame.

59- Kila kitu alichokiwajibishia Allaah kutoweka basi kitatoweka, isipokuwa Pepo, Moto, ´Arshi, Kursiy, Ubao Uliohifadhiwa, Kalamu na Parapanda. Hakuna kitu katika hivi kitachotoweka. Baada ya hapo Allaah atawafufua viumbe siku ya Qiyaamah katika ile hali waliyofikia. Atawafanyia hesabu vile Anavyotaka. Kundi litaingia Peponi na kundi lingine litaingia Motoni. Vilevile

---

kutoka kwake madhehebu haya. Maswahabah wengine wakamraddi ikiwa ni pamoja na ´Abdullaah bin ´Umar, ´Abdullaah bin ´Abbaas, Waathilah bin Asqaa´ na wengineo. Qadariyyah wamegawanyika makundi mawili:

Kundi la kwanza: Wanapinga kabisa kuwa Allaah alitangulia kuyajua mambo na wanadai kuwa Allaah hakuyakadiria mambo milele na hakutangulia kuyajua. Anayajua pale yanapotokea. Hawa ndio wale waliyopindukia.

Wanachuoni wamesema kuwa pote hili limetoweka na hawa ndio wale waliofanyiwa Takfiyr na maimamu kama Maalik, ash-Shaafi´iy na Ahmad. Hawa ndio wale ambao Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) alisema juu yao:

"Jadiliana na Qadariyyah kwa elimu. Wakiikubali watakuwa ni wenye kushindwa na wakiipinga basi wanakufuru."

Kundi la pili: Ni wale walioko kati kwa kati; Qadariyyah wa kawaida. Hawa wamekubali elimu na uandishi. Wameenda kinyume na Salaf pale waliposema kuwa matendo ya waja wameyakadiria wenyewe na ni yenye kujitokeza kutoka kwao kwa njia ya upekee. Kwa msemo mwingine wanachotaka kusema ni kuwa matendo ya waja hakuyataka Allaah na wala hakuyaumba na kwamba matakwa ya Allaah ni yenye kuenea isipokuwa tu matendo ya waja na kwamba aliyoumba Allaah ni yenye kuenea katika kila kitu isipokuwa tu matendo ya mja. Madhehebu haya, pamoja na kwamba ni madhehebu batili, lakini hata hivyo ni mepesi kuliko hayo ya kwanza." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (01/355-357)

Atawaambia viumbe vyengine vilivyobakia ambavyo havikuumbwa kwa ajili ya kubaki:

"Kuweni udongo!"

60- Kuamini kwamba kisasi kitakuwepo siku ya Qiyaamah kati ya viumbe wote; wanaadamu, wanyama pori, wadudu wanaotambaa mpaka sisimizi kwa sisimizi mwingne, mpaka Allaah (´Azza wa Jall) azichukue haki za baadhi kutoka kwa baadhi nyingine; watu wa Peponi kutoka kwa watu wa Motoni, watu wa Motoni kutoka kwa watu wa Peponi, kadhalika watalipana watu wa Peponi wenyewe kwa wenyewe na watu wa Motoni wenyewe kwa wenyewe.

61- Kuyatakasa matendo kwa ajili ya Allaah.

62- Kuridhia juu ya mipango ya Allaah na kuwa na subira juu ya hukumu za Allaah. Kuamini yale Allaah (´Azza wa Jall) aliyoyasema, makadirio ya Allaah yote, ya kheri na ya shari yake, matamu na machungu yake. Allaah aliyajua yale ambayo waja watayafanya na kule watakakokuwa. Hawatoki ndani ya Ujuzi wa Allaah. Hakukuwi kitu katika ardhi wala mbinguni isipokuwa kile Allaah (´Azza wa Jall) alichokijua. Tambua kuwa kile kilichokupata hakikukuwa cha kukukosa na kilichokukosa hakikuwa cha kukupata. Hakuna muumbaji aliye pamoja na Allaah (´Azza wa Jall).

63- Mtu anafanya Takbiyra nne[52] katika swalah ya jeneza. Haya ndio maoni ya Maalik bin Anas, Sufyaan ath-Thawriy, al-Hasan bin Swaalih, Ahmad bin Hanbal na Fuqahaa' wengine. Haya vilevile ndio maoni ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[53].

---

[52] Kusema "Allaahu Akbar".

[53] Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitangaza kifo cha an-Najaashiy ile siku aliyokufa. Baada ya hapo akatoka akaenda nao mahala pa kuswalia, wakapanga safu na wakamfanyia Takbiyra nne." (al-Bukhaariy (03/202) pamoja na "Fath-ul-Baariy" na Muslim (951))

Siraaj-ud-Diyn al-Hindiy amesema kuhusu maoni ya Abu Haniyfah, Maalik, ash-Shaafi´iy na Ahmad bin Hanbal juu ya idadi ya Takbiyra wakati wa swalah ya jeneza:

"Wote wanaonelea kuwa idadi ya Takbiyra kwa maiti ni nne." (Zubdat-ul-Ahkaam (135)).

64- Kuamini kuwa kila tone [la mvua] linaloshuka kutoka juu liko pamoja na Malaika mpaka litue pale alipoamrisha Allaah (´Azza wa Jall)[54].

65- Kuamini kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pindi alipowazungumzisha washirikina waliotupwa kisimani siku ya Badr walikuwa wakiyasikia maneno yake.

66- Kuamini kuwa mtu anapokuwa mgonjwa basi Allaah anamlipa kwa maradhi hayo[55].

67- Allaah anamlipa shahidi kwa kuuawa.

68- Kuamini kuwa watoto wanaposibiwa na kitu [cha kuumiza] hapa duniani wanaumia. Bakr bin Ukht ´Abdil-Waahid[56] amesema: "Hawaumii." Amesema uongo.

69- Tambua kwamba hakuna yeyote atayeingia Peponi isipokuwa kwa huruma wa Allaah na Allaah hatomuadhibu yeyote isipokuwa kwa kiwango cha madhambi yake. Lau Allaah angeliwaadhibu walioko mbinguni, walioko ardhini, wema na waovu wao, basi Angelikuwa ni mwenye kuwaadhibu pasi na kuwadhulumu. Haijuzu kumwambia Allaah (Tabaarak wa Ta´ala): "Ni mwenye kudhulumu." Mwenye kudhulumu ni yule mwenye kuchukua kisichokuwa chake, ilihali Allaah (Jalla Thanaa´uh) viumbe na amri vyote viwili ni Vyake. Viumbe ni Wake na ulimwengu pia ni Wake. Haulizwi kwa kile anachokifanya na wao [viumbe] wataulizwa. Hakusemwi: "Kwa nini?" wala "Vipi?". Asiwepo yeyote atayeingia kati ya Allaah na viumbe Wake.

---

[54] Haya yamesemwa na Imaam al-Hakam bin ´Utaybah na Imaam al-Hasan al-Baswriy (Rahimahumaa Allaah). Kuhusu maneno ya al-Hakam, yanapatikana "al-´Adhamah" (493) ya Imaam Abush-Shaykh (Rahimahu Allaah) na pia "Jaami´-ul-Bayaan ´an Ta´wiyl Aay-il-Qur-aan" (14/19) ya Imaam at-Twabariy. Kuhusu maneno ya al-Baswriy, yanapatikana pia "al-´Adhamah" (761).

[55] Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Hakuna Muislamu anayepatwa na maumivu isipokuwa Allaah humfutia makosa yake kama jinsi jani linavyoanguka chini kutoka kwenye mti." (al-Bukhaariy (10/110) pamoja na "Fath-ul-Baariy" na Muslim (2571))

[56] Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Ni mmoja katika viongozi wakubwa wa Mu´tazilah. Tazama wasifu wake katika "al-Miyzaan" (02/60-61)." (Taaliki ya Shar-us-Sunnah (68)).

70- Ukimsikia yoyote anayasema vibaya mapokezi[57] na wala hayakubali au anapinga kitu katika maelezo ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi utuhumu Uislamu wake. Huyo ni mtu aliye na maoni na madhehebu maovu[58]. Hakufanya jengine zaidi ya kumtukana Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake, kwa sababu tumemjua Allaah, Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Qur-aan, kheri na shari pamoja na dunia na Aakhirah kupitia mapokezi.

71- Qur-aan ni yenye kuihitajia Sunnah zaidi kuliko Sunnah inavyoihitajia Qur-aan[59].

72- Maneno, mijadala na magomvi, na khaswa inapokuja katika Qadar, ni jambo limekatazwa kwa mujibu wa mapote yote, kwa sababu Qadar ni siri ya Allaah. Kadhalika Mola (Tabaarak wa Ta´ala) amewakataza Mitume kuzungumza juu ya Qadar. Vilevile Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza kuzozana juu ya Qadar. Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Taabi´uun[60] walilichukia hilo. Vivyo hivyo ndivyo walivyofanya wanachuoni na wanyenyekevu. Wao pia walikataza kujadiliana juu ya Qadar. Kwa hivyo ni juu yako kujisalimisha,

---

[57] Uchache ni Athar. Wingi ni Aathaar. Imaam Muhammad bin Swaalih bin ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema:

"Athar ni kile chenye kunasibishwa kwa Swahabah au aliyekuja baada ya Swahabah (Taabi´iy). Kadhalika inaweza kuwa na maana kile chenye kunasibishwa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa sharti mtu aseme kwa mfano: "Imepokelewa katika Athar kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)."" (Mustwalah-ul-Hadiyth, uk. 07)

[58] Imaam Ahmad bin Hanbal (Rahimahu Allaah) amesema:

"Yule ambaye anarudisha Hadiyth moja ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) basi yuko katika ukingo wa uharibifu." (al-Ibaanah al-Kubraa (01/97) ya Ibn Battwah)

[59] al-Fudhwayl bin Ziyaad amesema:

"Nilimsikia Abu ´Abdullaah - yaani Ahmad bin Hanbal - akiulizwa kuhusu Hadiyth inayosema kwamba Sunnah inaihukumu Qur-aan. Akasema: "Sithubutu kusema kuwa Sunnah inaihukumu Qur-aan, lakini uhakika wa mambo ni kwamba Sunnah inaifasiri na kuiweka wazi Qur-aan." (al-Jaami´, uk. 191-192, ya Ibn ´Abdil-Barr)

[60] Uchache ni Taabi´iy. Wingi ni Taabi´uun. Imaam al-Khatwiyb al-Baghdaadiy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Taabi´iy ni yule aliyesuhubiana na Maswahabah." (al-Kifaayah, uk. 59)

kuthibitisha na kuamini yale aliyosema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu ya jumla ya mambo na kunyamazia yasiyokuwa hayo.

73- Kuamini kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisafirishwa usiku kuelekea mbinguni na akafika katika ´Arshi. Akazungumza na Allaah (Tabaarak wa Ta´ala), akaingia Peponi na akauona Moto. Akawaona Malaika na akayasikia maneno ya Allaah (´Azza wa Jall). Alikusanyiwa Mitume. Akaona ukingo wa ´Arshi na Kursiy na vyote vilivyomo mbinguni na ardhini hali ya kuwa yumacho. Jibriyl ndiye alimbeba juu ya Buraaq[61] mpaka akafika mbinguni. Katika usiku huo ndio alifaradhishiwa swalah na akarudi Makkah katika usiku huo huo. Hayo yalipitika kabla ya Kuhajiri.

74- Tambua kuwa roho za mashahidi zimo kwenye taa chini ya ´Arshi na zinaogelea Peponi. Roho za waumini ziko chini ya ´Arshi na roho za makafiri na watenda maovu ziko Barahuut[62] ambayo iko katika Sijjiyn[63].

75- Kuamini kuwa maiti hukalishwa ndani ya kaburi lake. Allaah humtumia roho ili Munkar na Nakiyr waweze kumuhoji kuhusu imani na mambo yake ya wajibu. Baada ya hapo roho yake inatolewa bila ya maumivu. Maiti hujua pindi mgeni anapokuja kumtembelea. Muumini huneemeshwa ndani ya kaburi lake na kafiri huadhibiwa vile Allaah anavyotaka.

76- Tambua kuwa harakati za migongo ya mbingu zinakuwa kwa mujibu wa mipango na makadirio ya Allaah.

---

61 Anas bin Maalik (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Buraaq aliletwa kwangu; ni mnyama ambaye ni mrefu kidogo kuliko punda na mfupi kidogo kuliko nyumbu." (Muslim)

62 Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Ni kisima kirefu kabisa kilichopo Hadhramawt (mji uliopo Yemen) ambapo rindi lake mtu hawezi kulifikia, kama ilivyotajwa katika chanzo cha kale (yaani "an-Nihaayah" (01/122)) ya Ibn Kathiyr. Hadiyth inayosema kuwa roho za makafiri ziko kwenye kisima Baraahuut sio Swahiyh jambo ambalo mara nyingi unaweza kuliona katika "ar-Ruuh" (uk. 145-147) ya Ibn-ul-Qayyim na pia "Ahwaal-ur-Ruuh" (uk. 255-263) ya Ibn Rajab." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (74))

63 Imaam ´Abdur-Rahmaan bin Naaswir as-Sa´diy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Sijjiyn. Ni mahala pa kubana na pa tabu kabisa. Imesemekana vilevile kuwa "Sijjiyn" ni chini katika ardhi ya saba na makazi ya watenda madhambi na makazi huko Aakhirah." (Taysiyr al-Kariym ar-Rahmaan, uk. 846)

77- Kuamini kwamba Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) ndiye ambaye alimzungumzisha Muusa bin Maryam siku ya Twuur. Muusa aliyasikia maneno kutoka kwa Allaah kwa sauti iliyoingia katika masikio yake na si kutoka kwa mwengine. Mwenye kusema yasiyokuwa haya basi amemkufuru Allaah Mtukufu[64].

78- Akili ni yenye kuzaliwa. Kila mtu amepewa akili kwa kiwango alichokitaka Allaah. Wanatofautiana katika akili kama mfano wa atomi kwenye mbingu. Kila mtu anatakiwa kutenda kwa kiasi na akili aliyompa Allaah. Akili haichumwi, bali ni fadhila kutoka kwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

79- Tambua ya kwamba Allaah amewafadhilisha baadhi ya waja juu ya wengine katika dini na dunia kutokana na uadilifu Wake. Hakusemwi: "Amedhulumu na kupendelea." Mwenye kusema: "Fadhila za Allaah kwa muumini na kafiri ni sawa sawa" ni mtu wa Bid´ah. Bali uhakika wa mambo ni kuwa Allaah amewafadhilisha waumini juu ya makafiri, mtiifu juu ya mtenda maasi na aliyelindwa na makosa juu ya mwenye kunyimwa nusura. Ni kutokana na uadilifu Wake na ni fadhila Anazompa amtakaye na Anamnyima amtakaye.

80- Haijuzu kuwaficha waislamu nasaha - ni mamoja wakawa wema au waovu - inapokuja katika mambo ya dini. Mwenye kufanya hivo basi atakuwa amewadanganya waislamu, yule mwenye kuwadanganya waislamu atakuwa ameidanganya dini na mwenye kuidanganya dini basi atakuwa amemfanyia Allaah khiyana, Mtume Wake na waumini.

81- Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) ni Mwenye kusikia na kuona, Mwenye kusikia na mjuzi. Mikono Yake miwili ni yenye kukunjuliwa. Allaah alijua kuwa viumbe Wake watamuasi kabla ya kuwaumba. Elimu Yake ni yenye kupita kwao. Elimu Yake haikumzuia kuwaongoza katika Uislamu na kuwatunuku kwa sababu ya ukarimu na fadhila Zake - himdi zote zinamstahikia Yeye.

---

[64] Imaam ´Abdullaah bin Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Nilimsikia Abu Ma´mar al-Hudhaliy akisema: "Ambaye anadai kuwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) hazungumzi, hasikii, haoni, hakasiriki wala haridhii basi hamwamini Allaah (Tabaarak wa Ta´ala). Ukimuona amesimama karibu na kisima, basi msukume ndani yake. Haya ndio ambayo ninamuabudu Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) kwayo kwa sababu hawamuamini Allaah (Tabaarak wa Ta´ala)."" (as-Sunnah (532)).

82- Tambua ya kwamba kuna bishara tatu wakati wa kufa. Kunasemwa: "Furahi, ewe kipenzi cha Allaah kwa radhi na Pepo ya Allaah!" Kunasemwa pia: "Furahi, ewe adui wa Allaah kwa ghadhabu na Moto wa Allaah!" Kunasemwa vilevile: "Furahi, ewe mja wa Allaah kwa Pepo baada ya Uislamu!" Haya yamesemewa na Ibn ´Abbaas.

83- Tambua kuwa wa kwanza atayemuona Allaah (Ta´ala) Peponi ni kipofu, kisha wanaume halafu wanawake kwa macho ya vichwani mwao, kama alivyosema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu kama mnavyouona mwezi katika usiku wa mwezi mweupe - hamtosongamana katika kumuona."[65]

Kuamini haya ni wajibu na kuyapinga ni kufuru.

84- Tambua ya kwamba haukuwepo uzandiki, ukafiri, shaka, Bid´ah, upotevu wala kutatizika katika dini isipokuwa ni kwa sababu ya elimu ya falsafa na wanafalsafa, mijadala, mizozo na magomvi. Ajabu iliyoje kuona namna ambavyo mtu anathubutu kujishughulisha na mijadala, mizozo na magomvi ilihali Allaah (Ta´ala) anasema:

مَا يُجَادِلُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا

"Habishani katika *Aayaat* za Allaah isipokuwa wale waliokufuru."[66]

Kwa hivyo ni lazima kwako kujisalimisha, kuridhia juu ya mapokezi na wapokezi, kukomeka pamoja na kunyamaza.

85- Kuamini kuwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) atawaadhibu viumbe Motoni kwenye minyororo na pingu na hali Moto uko ndani yao, juu yao na chini yao. Haya (yanatajwa) kwa sababu Jahmiyyah - mmoja wao ni Hishaam al-Fuutwiy[67] - amesema:

"Allaah atawaadhibu watu mbele ya Moto."

---

[65] al-Bukhaariy (554) na (574) na Muslim (633).

[66] 40:04

[67] Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Alikuwa ni jamaa wa Ibn-ul-Hudhayl na alikuwa akiita katika madhehebu ya Mu´tazilah." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (85))

Huku ni kupingana na Allaah na Mtume Wake.

86- Tambua ya kwamba swalah za faradhi ni tano. Hakuzidishwi juu yake na wala nyakati zake hazipunguzwi. Katika safari kunaswaliwa Rakaa´ mbili isipokuwa tu swalah ya Maghrib. Mwenye kusema kuwa ni zaidi ya swalah tano, amezua, na mwenye kusema kuwa ni chini ya tano, amezua. Allaah hakubali kitu katika swalah hizo isipokuwa kwa wakati wake, isipokuwa endapo mtu atakuwa ni mwenye kusahau, hapo atakuwa ni mwenye kupewa udhuru. Hivyo basi, aiswali pale atapokuikumbuka. Kama mtu ni msafiri anaweza kujumuisha baina ya swalah mbili akipendelea kufanya hivo.

87- Zakaah inatolewa katika dhahabu, fedha, matunda na nafaka, kutokana na vile alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kama ataigawa mwenyewe inafaa kufanya hivo na akimpa kiongozi inafaa vilevile kufanya hivo.

88- Tambua ya kwamba kitu cha kwamza katika Uislamu ni Shahaadah: ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake.

89- Yale Allaah aliyosema ni kama alivyosema na hakuna mgongano katika yale aliyosema. Nayo ni kwa yule aliyosema.

90- Kuamini Shari´ah yote.

91- Tambua ya kwamba biashara inayoendelea katika masoko ya waislamu ni halali ilimradi vimejengwa kwa mujibu wa hukumu ya Qur-aan, Uislamu na Sunnah, bila ya kuingiliwa na ubadilishaji, dhuluma, ukandamizaji, khiyana au kwenda kinyume na Qur-aan au kinyume na yale yanayojulikana kwa jumla.

92- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba inatakiwa kwa mja siku zote awe na woga muda wakuwepo katika dunia hii, kwa sababu hajui atakufa katika hali gani, atahitimisha kwa kitu gani na atakutana na Allaah (´Azza wa Jall) na lepi, hata kama atafanya matendo yote ya kheri.

93- Inatakikana kwa mtu mwenye kuifanyia israfu nafsi yake kutokata matumaini yake kwa Allaah (Ta´ala) wakati wa kufa, anatakiwa kumjengea dhana nzuri Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) na akhofu juu ya dhambi zake. Endapo Allaah atamrehemu, inatokamana na fadhila Zake, na endapo Atamuadhibu, inatokamana na dhambi Zake.

94- Kuamini ya kwamba Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) alimfanya Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuyajua yatayokuwepo katika Ummah wake mpaka siku ya Qiyaamah.

95- Tambua kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ummah wangu utafarikiana katika mapote sabini na tatu. Yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu." Nao ni al-Jamaa´ah. Kukasemwa: "Ee Mtume wa Allaah! Ni kina nani hao?" Akasema: "Ni wale wataokuwemo katika yale niliyomo mimi hii leo na Maswahabah zangu."[68]

Dini ilikuwa katika hali hii mpaka katika ukhalifah wa ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh). Hali kadhalika ndivyo hali ilivyokuwa katika zama za ´Uthmaan. Pindi alipouawa ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh) ndipo kukaja tofauti na Bid´ah. Watu wakawa mapote na makundi. Hata hivyo kuna watu waliokuwa imara katika haki katika kile kipindi cha kwanza cha mabadiliko; wakazungumza kwayo, wakaitendea kazi na wakawalingania watu kwayo. Hali ikaendelea kuwa nzuri mpaka ilipofika katika zama za nne katika ukhalifah wa watu fulani. Ndipo zama zikabadilika, watu wakabadilika sana, Bid´ah zikaenea na wakakithiri walinganizi wanaolingania katika isiyokuwa njia ya haki na al-Jamaa´ah na kukapatikana mitihani katika kila jambo ambalo hakulizungumzia si Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala Maswahabah zake. Wakalingania katika mfarakano - ilihali Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza mfarakano - na baadhi wakawakafirisha wengine. Kila mmoja akawa analingania katika maoni yake na huku anamkufurisha yule mwenye kwenda kinyme naye. Matokeo yake wajinga, watu wa kawaida na watu wasiokuwa na elimu wakapotea. Wakawatamanisha watu na mambo ya kidunia na wakawatishia na adhabu za dunia. Hivyo watu wakawafuata kwa kuogopa juu ya dunia yao na kwa ajili ya kuipenda dunia yao. Sunnah na watu wake wakawa ni wenye kujificha. Bid´ah ikadhiri na kuenea. Wakakufuru pasi na kujua kwa njia mbali mbali. Wakatendea kazi kipimo (Qiyaas). Wakafasiri uwezo wa Allaah, Aayah, hukumu, maamrisho na makatazo Yake kwa mujibu wa akili na mitazamo yao. Yale yenye kuafikiana na akili zao wakakubalinaa nayo na yale

[68] at-Tirmidhiy (2779) na al-Haakim (01/129).

yasiyoafikiana na akili zao wakayarudisha. Uislamu ukawa mgeni, Sunnah ikawa geni na Ahl-us-Sunnah wakawa ni wageni majumbani mwao.

96- Tambua ya kwamba Mut´ah[69] na Istihlaal[70] ni haramu mpaka siku ya Qiyaamah.

97- Fahamu kuwa Banuu Haashim wana fadhila zao kwa sababu ya udugu wao pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Tambua fadhila za Quraysh, waarabu na makabila mengine yote. Zijue nafasi zao na haki zao katika Uislamu. Aliyeachwa huru na watu ni katika wao. Zijue haki za watu wengine katika Uislamu. Zitambue fadhila za Wanusuraji na wasia wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu yao. Hali kadhalika familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) - usiisahau! Zitambue fadhila na utukufu wao. Vilevile majirani wake al-Madiynah - zitambue fadhila zao!

98- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba wanachuoni bado ni wenye kuendelea kuraddi maoni ya Jahmiyyah mpaka ilipofika katika ukhalifah wa watu fulani. Hapa ndipo Ruwaybidhwah walipoanza kuzungumzia katika mambo yanayowahusu watu wote. Wakatukana mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wakachukua vipimo na maoni. Wakawakafirisha wenye kwenda kinyume nao. Hivyo mjinga na mghalilikaji akajipenyeza katika maneno yao na akafanya hivo yule asiyekuwa na elimu mpaka wakakufuru pasi na kujua. Ummah ukaangamia kwa mitazamo mbali mbali, wakakufuru kwa mitazamo mbali mbali, wakaingia katika uzandiki kwa mitazamo mbali mbali, wakapotea kwa mitazamo mbali mbali na wakafarikiana na kuzua kwa mitazamo mbali mbali, isipokuwa yule aliyekuwa imara juu ya maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), maamrisho yake na maamrisho ya Maswahabah zake. Hakumtia makosani yeyote katika wao na hakulivuka jambo lao. Yaliyowatosheleza yakamtosheleza na yeye na wala akawa hakutamani isiyokuwa njia na

[69] Ndoa za muda fulani kwa lengo la kustarehe na kukidhi haja. ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku ya Khaybar aliharamisha ndoa ya Mu´tah na kula nyama ya punda wa kufuga." (al-Bukhaariy (4216))

[70] Ndoa ili yule mume wa kwanza aweze kumuoa tena yule mwanamke ambaye kishamtaliki mara tatu hapo kabla. ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Laana ya Allaah iwe juu ya yule ambaye anamuoa mwanamke ili amfanye kuwa ni halali kwa yule mume wake wa kwanza." (Abu Daawuud (2076) na at-Tirmidhiy (1128))

madhehebu yao. Akajua kuwa wao ndio walikuwa wakifuata Uislamu na imani sahihi. Matokeo yake akawafuata katika dini yake na akastarehe. Anatambua kuwa dini ina maana ya kuwafuata Maswahabah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

99- Tambua kuwa yule mwenye kusema:

"Matamshi ya Qur-aan yameumbwa."

ni Mubtadi´. Mwenye kunyamaza na asisemi kuwa yameumbwa wala hayakuumbwa, ni Jahmiy. Hivi ndivyo alivyosema Ahmad bin Hanbal. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Hakika yule atakayeishi katika nyinyi baada yangu, basi atakuja kuona tofauti nyingi. Tahadharini na mambo ya kuzua, kwani hakika ni upotevu. Jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu. Ziumeni kwa magego yenu."[71]

100- Tambua kuwa maangamivu ya Jahmiyyah yamekuja kwa sababu ya kumfikiria Mola (´Azza wa Jall) na matokeo yake wakaingiza "Kwa nini?" na "Vipi?". Wakaacha mapokezi na wakaweka kipimo. Hivyo wakawa wameilinganisha dini na akili zao. Ndipo wakaleta ukafiri wa wazi usiojificha. Wakawakafirisha viumbe na wakawa ni wenye kutenzwa nguvu, ndipo wakaanza kuzungumza kwa ukanushaji[72].

101- Baadhi ya wanachuoni - mmoja wao ni Ahmad bin Hanbal (Radhiya Allaahu ´anh) - wamesema:

"Jahmiy ni kafiri. Sio katika waislamu. Damu yake ni halali. Hafai kurithi wala kurithiwa. Haya ni kwa sababu anasema: "Hakuna swalah ya Ijumaa, swalah ya mkusanyiko, swalah mbili za ´Iyd wala zakaah."

Wamesema:

"Mwenye kusema kuwa Qur-aan haikuumbwa ni kafiri."

---

[71] Abu Daawuud (4602) na at-Tirmidhiy (2676). at-Tirmidhiy amesema: "Hadiyth ni nzuri na Swahiyh."

[72] Imaam ´Abdul-´Aziyz bin Baaz (Rahimahu Allaah) amefafanua neno "ukanushaji" (Ta´twiyl) namna hii:

"Maana yake ni kuikanusha sifa, kuipindisha au kupindisha maana yake." (Shar al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 17)

Wakahalalisha upanga juu ya Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wakaenda kinyume na waliokuwa kabla yao. Wakawapa watu mtihani kwa kitu ambacho hakikuzungumzwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala yeyote katika Maswahabah zake. Wakataka kuitokomeza misikiti na sehemu za kuswalia. Wakaudhoofisha Uislamu. Wakaibwetesha Jihaad na wakatenda kwa ajili ya mfarakano. Wakaenda kinyume na mapokezi na wakazungumza kwa yaliyofutwa. Wakatumia hoja kwa Aayah zisizokuwa wazi na hapo ndipo wakawafanya watu kutilia shaka maoni yao na dini yao. Wakagawanyika juu ya Mola Wao. Wakasema:

"Hakuna adhabu ndani ya kaburi, hakuna Hodhi, hakuna Uombezi wala Pepo na Moto havijaumbwa."

Wakapinga mengi katika yaliyosemwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ndipo wakahalalisha waliyohalalisha kuwakufurisha na damu zao kwa mtazamo huu. Yule mwenye kukanusha Aayah katika Kitabu cha Allaah, basi amekanusha Kitabu chote[73], na yule mwenye kukanusha moja katika mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), amekanusha mapokezi yote na hivyo ni mwenye kumkufuru Allaah Mtukufu. Kukapita kwao muda. Wakapata msaada wa mfalme katika hilo na wakauweka upanga na bakora chini ya hilo. Elimu ya Sunnah na al-Jamaa´ah ikachakaa na wakazidhoofisha. Zote mbili zikawa ni zenye kufichikana kwa sababu ya kudhiri kwa Bid´ah na falsafa na kwa sababu ya wingi wao. Wakachukua vikao vya elimu, wakadhihirisha maoni yao na wakaandika vitabu juu yavyo. Wakawapendekeza watu na wakawatafutia uongozi. Ikawa ni fitina kubwa kweli kweli. Hakuna aliyesalimika nayo isipokuwa yule aliyekingwa na Allaah. Dogo ambalo mtu alikuwa anaweza kukumbana nalo katika vikao vyao vya elimu, ni kuanza kuishuku dini yake, kuwafuata au kudai kuwa wako katika haki, na wakati huo huo yeye hajui kuwa yuko katika haki au batili. Matokeo yake anakuwa ni mwenye mashaka. Watu wakaangamia mpaka yalipofika masiku ya Ja´far - ambaye vilevile anaitwa al-Mutawakkil. Allaah akamfanya akaweza kuizima Bid´ah na kuidhihirisha haki. Kupitia kwake Ahl-us-Sunnah wakaweza kudhihiri na maneno yao

[73] ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Mwenye kukanusha herufi yake [ya Qur-aan] moja, basi amekanusha zote ndani yake." (Ibn Abiy Shaybah (01/102) na (10/513) na "Jaami´-ul-Bayaan ´an Ta´wiyl Aay-il-Qur-aan" (56) ya at-Twabariy).

yakaenea pamoja na kuwa walikuwa wachache na Ahl-ul-Bid´ah ndio walikuwa wengi. Hali iko hivyo mpaka hii leo.

Rasm[74] na alama za upotevu bado vimebaki na kuna watu wanayatendea kazi na kulingania kwavyo. Hakuna anayewakataza na hakuna mwenye kuwazuia kwa yale wanayoyasema na kuyafanya!

102- Tambua kuwa hakukuja Bid´ah yoyote isipokuwa inatoka kwa watu duni, wapumbavu na wafuasi wa kila mwenye kupiga ukelele. Wanaenda na kila upepo. Ambaye hali yake ni kama hii, basi hana dini yoyote. Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) amesema:

فَمَا اخْتَلَفُوا إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ

"Basi hawakukhitilafiana isipokuwa baada ya kuwajia elimu kwa uhusuda baina yao."[75]

Kadhalika:

وَمَا اخْتَلَفَ فِيهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ

"Hawakukhitilafiana katika hayo isipokuwa wale waliopewa baada ya kuwajia hoja bayana kwa uhusuda baina yao."[76]

Hawa ni wale wanachuoni waovu na watu wa matamanio na wa Bid´ah.

103- Tambua ya kwamba siku zote kutaendelea kuwepo kikundi kutoka katika Ahl-ul-Haqq was-Sunnah[77]. Allaah atawaongoza na awaongoze wengine kupitia wao. Kupitia wao Ataihuisha Sunnah. Hao ndio wale Allaah (Ta´ala) aliowaelezea pamoja uchache wao wakati wa kutofautiana. Amesema:

فَمَا اخْتَلَفُوا إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ

74 Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Rasm ni istilahi ya Suufiyyah na kwa mujibu wao ni sifa inayopitika katika elimu Yake (Ta´ala) iliyotangulia na imegawanyika sehemu mbili; kamilifu na pungufu." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (101)).

75 45:17

76 02:213

77 Watu wa haki na Sunnah.

"Basi hawakukhitilafiana isipokuwa baada ya kuwajia elimu kwa uhusuda baina yao."

Kisha Akawavua wao na kusema:

فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا لِمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ ۗ وَاللَّهُ يَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ

"Ndipo Allaah Akawaongoza wale walioamini kuendea haki katika yale waliyokhitilafiana kwa idhini Yake - na Allaah Humwongoza Amtakaye katika njia iliyonyooka."[78]

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Kikundi katika Ummah wangu kitaendelea siku zote kuwa ni chenye kushinda katika haki. Hakitodhurika na wale wenye kuwapinga mpaka ifike amri ya Allaah ilihali bado ni wenye kushinda."[79]

104- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba elimu sio mtu kuwa na mapokezi na vitabu vingi, isipokuwa mwanachuoni ni yule mwenye kufuata elimu na Sunnah, ijapokuwa atakuwa na elimu na vitabu vichache. Yule mwenye kwenda kinyume na Kitabu na Sunnah, basi huyo ni mtu wa Bid´ah. Haijalishi kitu hata kama atakuwa na mapokezi na vitabu vingi.

105- Tambua - Allaah akurehemu - yule mwenye kusema katika dini ya Allaah kwa maoni, kipimo na tafsiri yake bila ya kuwa na dalili kutoka katika Sunnah na al-Jamaa´ah, atakuwa amesema juu ya Allaah asichokijua. Na yule mwenye kusema juu ya Allaah asichokijua, huyo ni katika wenye kujikalifisha[80].

106- Haki ni ile ambayo imekuja kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall). Sunnah ni njia ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). al-Jamaa´ah ni ile waliyokusanyikaemo Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika ukhalifah wa Abu Bakr, ´Umar na ´Uthmaan.

[78] 02:213

[79] Muslim (1924)

[80] Imaam Ibn Abiy-´Izz al-Hanafiy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Anayezungumza pasi na elimu hafuati jengine isipokuwa matamanio yake." (Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah, uk. 385)

107- Ambaye atatosheka na Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yale Maswahabah zake na al-Jamaa´ah wanayofuata, atawashinda Ahl-ul-Bid´ah wote, utastarehe mwili wake na dini yake itasalimika - Allaah akitaka. Haya ni kwa sababu Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ummah wangu utafarikiana."

Na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawa ametubainishia lenye kuokoka katika wao. Akasema:

"Ni wale wataokuwemo katika yale niliyomo mimi hii leo na Maswahabah zangu."[81]

Hii ndio dawa na ubainifu, jambo la wazi na mnara unaotoa nuru. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Tahadharini na kupetuka mipaka na yale yenye kuvuka mipaka, na jilazimianeni na dini yenu ya kale."[82]

108- Tambua kuwa dini ya kale ni tangu alipokufa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mpaka alipouawa ´Uthmaan bin ´Affaan (Radhiya Allaahu ´anh). Kuuawa kwake ndio ilikuwa chanzo cha mfarakano na tofauti. Ummah wa Kiislamu ukapigana vita na kufarikiana na hivyo ukafuata matamanio na hawaa. Ukaanza kumili kwenye dunia. Hakuna yeyoye aliye na rukhusa ya kuzua kitu katika mambo ambayo hawakuwemo Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kadhalika inahusiana na mtu mwenye kulingania katika kitu kilichozushwa na Ahl-ul-Bid´ah kabla yake. Mtu huyo ni kama yule aliyekizusha. Mwenye kudai hivyo au akazungumza kwalo, ameirudisha Sunnah na kwenda kinyume na haki na al-Jamaa´ah. Ameruhusu Bid´ah na atakuwa ni muovu katika Ummah huu kuliko Ibliys.

109- Mwenye kuzijua zile Sunnah ambazo watu wa Bid´ah wameziacha na kuzikhalifu na yeye akawa ameshikamana nazo, huyo ni mtu wa Sunnah na

---

[81] at-Tirmidhiy (2641)

[82] ´Abdur-Razzaaq (10/252), ad-Daarimiy (01/50), Ibn Naswr al-Marwaziy katika "as-Sunnah" (85) na wengineo. ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Haya ni maneno ya ´Abdullaah bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) na sio ya Mtume wa Allaah (Swalal Allaahu ´alayhi wa sallam)." (Mkanda "Sharh-us-Sunnah" (06))

mtu wa al-Jamaa´ah. Ana haki ya kufuatwa, kusaidiwa na kuhifadhiwa na mtu huyo ni katika watu waliopendekezwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

110- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba misingi ya Bid´ah ni milango mine. Katika milango hii mine yakatoka matawi sabini na mbili. Halafu baada ya hapo kila Bid´ah katika hizi ikatoa matawi mpaka zote zikafikia maoni elfu mbili na mia nne. Zote ni upotevu na zote ni Motoni isipokuwa moja tu: ni yule mwenye kuamini yale yaliyomo katika kitabu hichi na akayaamini pasi na kuwa na shaka na wasiwasi ndani ya moyo wake. Huyo ndiye mtu wa Sunnah na ndiye mwenye kuokoka - Allaah akitaka.

111- Tambua - Allaah akurehemu - lau watu wangelijiepusha na mambo ya kuzua, wasiyavuke na kitu na wasizalishe maneno ambayo hakukupokelewa mapokezi kwayo kutoka kwa Mutme wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wala Maswahabah zake, basi kusingelikuwepo Bid´ah yoyote.

112- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba hakuna kizuizi baina ya mja na hali yake kama muumini yenye kumfanya kuwa kafiri, isipokuwa ikiwa atakanusha kitu katika yale aliyoteremsha Allaah (Ta´ala), akazidisha au akapunguza katika maneno ya Allaah au akapinga kitu katika aliyosema Allaah (´Azza wa Jall) au kitu katika alichokisema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mche Allaah - Allaah akurehemu - na itazame nafsi yako. Tahadhari na kupetuka mipaka katika dini, kwani hakika ni jambo halina lolote kuhusiana na njia ya haki.

113- Yote niliyokueleza katika kitabu hichi yanatoka kwa Allaah (Ta´ala), kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Maswahabah zake, kutoka kwa Taabi´uun na kutoka katika karne ya tatu na karne ya nne. Mja wa Allaah! Mche Allaah! Ni juu yako kusadikisha, kujisalimisha, kutegemeza[83] na kuridhia yaliyomo ndani ya kitabu hichi. Usimfiche Muislamu yoyote kitabu hichi. Huenda Allaah akamrudisha aliyechanganyikiwa kutoka katika kuchanganyikiwa, mtu wa Bid´ah kutoka katika Bid´ah zake au mpotevu kutoka katika upotevu wake na akaokoka

[83] ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Anachokusudia ni kwamba usizue kitu kutoka kwako mwenyewe. Hakumaanishwi utegemezi "Tafwiydhw" waliyomo Mufawwidhwah." (Sharh-us-Sunnah, uk. 321)

nacho[84]. Mche Allaah na shikamana na jambo la kwanza na la kale[85] ambalo nimekueleza katika kitabu hichi. Allaah amrehemu mja na awarehemu wazazi wake aliyekisoma kitabu hichi, akakieneza, akakitendea kazi, akalingania kwacho na akakitumia kama hoja. Kwani hakika ni dini ya Allaah na ni dini ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kuhalalisha kitu chenye kwenda kinyume na yaliyomo ndani ya kitabu hichi, hakika atakuwa si mwenye kumuabudu Allaah kwa dini yoyote. Atakuwa ameyarudisha yote kama mfano wa mtu mwenye kuamini yote aliyosema Allaah (Tabaarak wa Ta´ala), lakini akaitilia shaka herufi moja. Kwa hiyo atakuwa ameyarudisha yote aliyosema Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) na hivyo ni kafiri. Kama ambavyo kushuhudia ya kwamba "hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah" haikubaliwi kwa mwenye kuitamka isipokuwa kwa kuwa na nia ya kweli na kuitakasa yakini, kadhalika Allaah hakubali kitu katika Sunnah ikiwa mtu ataacha baadhi yake. Yule mwenye kuacha kitu katika Sunnah basi atakuwa ameiacha Sunnah yote. Jilazimie na kukubali na uache ubishi na wingi wa maneno kwa sababu mambo hayo hayana lolote kuhusiana na dini ya Allaah. Mche Allaah, hakika zama zako ni zama ovu.

114- Fitina ikitokea basi wewe jilazimie kuwa ndani ya nyumba yako na kimbia palipo jirani na fitina. Tahadhari na ushabiki. Aina zote za vita vya

[84] Amesema tena (Hafidhwahu Allaah) katika ukurasa huo huo akisherehesha maneno ya mwandishi:

"Ni juu yako kusadikisha na usikadhibishe kitu katika yaliyotajwa katika Kitabu hichi. Kwa sababu yamechukuliwa kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Hivyo ni juu yako kujisalimisha na usitilie shaka katika kuyachukua. Yafuate na usizembee... "

Akaendelea kusema tena (Hafidhwahu Allaah) katika ukurasa huo huo:

"Kieneze kitabu hiki na wasambazie waislamu ili wanufaike nacho. Huku ni katika kueneza elimu yenye manufaa na ni katika kuusiana juu ya haki. Mambo yanatakiwa kuwa namna hii kueneza vitabu vyenye manufaa na vyenye faida na khasa vitabu vya ´Aqiydah. Kila ambavyo kitabu kitakuwa ni cha kale ndivyo jinsi kitakuwa karibu na haki. Kwa sababu kinakuwa karibu na zile karne bora."

[85] ´Allaamah Swaalih al-Fawzaan (Hafidhwahu Allaah) amesema tena:

"Bi maana lazimiana na jambo la kale. Nalo ni yale aliyokuwa akifuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake na zile karne bora." (Sharh-us-Sunnah, uk. 322)

Halafu akasema tena (Hafidhwahu Allaah) katika ukurasa wa kufuata kutokana na maneno ambayo mwandishi ametaja hapo juu ambayo baadhi ya washereheshaji wamemkosoa na kusema eti amejisifu yafuatayo:

"Kuna baadhi ya washereheshaji wamemkosoa mwandishi na kusema kwamba amekitakasa kitabu chake. Tunasema kuwaambia kwamba huku sio kukitakasa kitabu chake. Bali huku ni kusisitiza juu ya kushikamana na mfumo wa Salaf, jambo ambalo limetajwa katika kitabu hichi na kwenye vyengine."

kidunia kati ya waislamu ni fitina. Mche Allaah, hali ya kuwa peke yake hana mshirika, na usiviendee, usipigane katika vita hivyo, usiwe upande wa yeyote, usijiunge na yeyote na wala usipende chochote katika mambo hayo, kwa sababu imesemwa: "Mwenye kupenda matendo ya watu - sawa ikiwa matendo hayo ni kheri au shari - ni kama mfano wa yule aliyefanya." Allaah atuwafikishe sisi na nyinyi katika yale anayoyaridhia na atuepushe na kumuasi.

115- Zitazame nyota kwa uchache iwezekanavyo[86], isipokuwa ikiwa kama unahitajia kujua msaada wa nyakati za swalah. Jiepushe na yote yasiyokuwa hayo, kwani hakika yanaita katika uzandiki.

116- Tahadhari na kutazama katika elimu ya falsafa na kukaa pamoja na watu wa falsafa.

117- Jilazimie mapokezi na watu wa mapokezi. Waulize wao, keti pamoja nao na chota kutoka kwao.

118- Tambua kuwa Allaah hajawahi kuabudiwa kama kuwa na khofu juu Yake. Njia za khofu, huzuni, huruma na haya zinatokamana na Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

119- Tahadhari kukaa pamoja na wanaoita katika shauku na mapenzi, wenye kukaa faragha pamoja na wanawake na kukaa kule wanakopita, hakika watu wote hawa wamo upotevuni.

---

[86] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema akifafanua maneno haya ya mtunzi:

"Kuna hali tatu za kutazama nyota:

Ya kwanza: Mtu akatazama nyota huku akiamini kuwa zinaleta taathiri mbalimbali katika ulimwengu. Hii ni shirki kubwa katika uola. Kadhalika hii ndio shirki ya watu wa Ibraahiym (´alayhis-Swalaatu was-Salaam).

Ya pili: Akatazama nyota na akadai kuwa anajua mambo yaliyofichikana (Ghayb). Mtu sampuli hii haamini kuwa nyota zina taathira, bali anaamini kuwa mwenye kuleta taathira ni Allaah lakini hata hivyo anadai kuwa anajua mambo yaliyofichikana kwa kutazamia nyota. Hii pia ni kufuru.

Ya tatu: Akatazama nyota ili aweze kujua Qiblah kilipo, wakati wa swalah, zimwelekeze njia anapokuwa nchikavu au baharini n.k. Hili ni sawa. Haya ndio maoni sahihi ya wanachuoni. Pamoja na hivyo kuna wanachuoni ambao wamelikataza." (Mkanda "Sharh-us-Sunnah" (07))

120- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) amewaita viumbe wote katika kumuabudu Yeye na amewaneemesha anaowataka katika Uislamu kutokana na fadhila Zake.

121- Mtu anatakiwa anyamazie kati ya vita vilivyopitika kati ya ´Aliy na Mu´aawiyah, ´Aaishah, Twahlah, az-Zubayr pamoja na wale waliokuwa pamoja nao[87]. Usijadiliane juu yao, liachie jambo lao kwa Allaah (Tabaarak wa

[87] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu tofauti iliyotokea kati ya Maswahabah:

"Na wanajitenga mbali na njia ya Raafidhwah, ambao wanawachukia na kuwatukana Maswahabah, hali kadhalika Nawaaswib, ambao wanawaudhi watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ima kwa kauli au matendo.

Na wanayanyamazia yaliyopitika baina ya Maswahabah na wanasema:

"Kati ya mapokezi haya yaliyopokelewa kuna ambayo ni ya uongo, na kuna ambayo yamezidishwa juu yake na kupunguzwa, na kuna ambayo yamebadilishwa kwa sura yake ya kihakika na ndani yake kuna ya sahihi ambayo wamepewa udhuru kwayo. Ima walikuwa ni wenye kujitahidi baada ya kuifikia haki wakapatia, au walikuwa ni wenye kujitahidi baada ya kuifikia haki wakakosea."

Wao pamoja na hivyo hawaitakidi ya kwamba kila mmoja katika Maswahabah kakingwa na dhambi kubwa au ndogo. Bali kinyume chake kuna uwezekano wakafanya dhambi kwa ujumla. Wana haki ya kutangulizwa na fadhila ambazo zinafanya wanasamehewa kwa lile wangelolifanya – ikiwa wamefanya kitu. Wanasamehewa hata madhambi ambayo yasingelisamehewa kwa mwengine yeyote baada yao, kwa kuwa wana mema mengi ambayo hana yeyote wa baada yao, na ambayo vilevile yanafuta makosa yao.

Kumethibiti kwa kauli ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba wao ndio karne bora na kwamba akitoa Swadaqah mmoja wao kiasi cha Mudd inauzito zaidi kuliko inayotolewa na aliye baada yao, hata kama huyu atatoa dhahabu sawa na kiasi cha mlima wa Uhud.

Ikiwa mmoja wao atapitikiwa na dhambi, atakuwa ima katubia kwa dhambi hiyo, au kaleta mema ambayo yameifuta au amesamehewa kwa fadhila za kutangulia kwake, au [kasamehewa] kwa uombezi wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) – na hakuna ambaye ana haki zaidi ya uombezi wake isipokuwa wao – au kapewa mtihani kwa majaribio ya duniani ambayo yamefuta dhambi yake. Ikiwa madhambi haya yaliyofanywa yanafanywa namna hii, vipi kwa mambo ambayo walikuwa ni wenye kujitahidi kuifikia haki?

Ikiwa wamepatia wana ujira mara mbili na wakikosea wana ujira mara moja na kosa lao limesamehewa. Isitoshe, matendo mabaya yaliyofanywa na baadhi yao ni machache mno na yasiyokuwa na maana ukilinganisha na fadhila za nafasi yao na mema yao, kama kwa mfano kumuamini Allaah na Mtume Wake,na kupigana Jihaad katika njia ya Allaah, Hijrah, nusra, elimu yenye manufaa na matendo mema n.k. Yule atakayetazana historia ya Maswahabah kwa elimu na umaizi na fadhila Alizowaneemesha Allaah kwazo, basi atajua kwa yakini ya kwamba wao ndio viumbe bora baada ya Mitume. Kamwe hakupatapo kuwepo na hakutokuwepo mtu mfano wao. Wao ndio wasomi wa wasomi katika Ummah huu – ambao

Ta´ala), hakika Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Tahadharini na kuwasema Maswahabah zangu na ndugu zangu wa ndoa."

Vilevile amesema:

"Hakika Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) amewatazama watu wa Badr akasema: "Fanyeni mtakalo. Mimi nimekusameheni.""[88]

122- Tambua - Allaah akurehemu - ya kwamba si halali kuichukua mali ya Muislamu, isipokuwa kile anachokitoa kwa hisia nzuri. Ikiwa mtu ana mali aliyoichuma kwa njia ilio ya haramu, ni jukumu lake. Si halali kwa yeyote kuchukua kitu kutoka kwake isipokuwa kwa idhini yake. Huenda mtu huyu akatubia na akataka kuirudisha kwa wenyewe, hivyo utakuwa umechukua kitu kilicho cha haramu.

123- Pato na chumo zinachukuliwa kutoka katika yale ambayo usalama wake umebainishwa. Ni halali kabisa isipokuwa tu yale ambayo ufisadi wake umedhihiri. Endapo ni fisadi, atachukua yale yenye kutimiza haja yake. Asisemi: "Ninaacha chumo na badala yake ninachukua vile ninavyopewa." Haya hayakufanywa na Maswahabah wala wanachuoni mpaka hii leo. ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Chumo lililo na sehemu ya uchafu ni bora kuliko kuwahitajia watu."[89]

124- Swalah tano zinajuzu nyuma ya yule unayeswali nyuma yake[90], isipokuwa ikiwa kama atakuwa mtu Jahmiy, hakika huyo ni mkanushaji[91].

ndio watu bora na wa karimu kwa Allaah (Ta´ala)." (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah, uk. 111-115 ya Imaam Ibn Baaz)

[88] al-Bukhaariy (3006) na Muslim (2494).

[89] Iswlaah-ul-Maal (321) ya Ibn Abiyd-Dunyaa.

[90] ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Rahimahu Allaah) amesema pindi alipokuwa akisherehesha maneno ya Imaam at-Twahaariy ifuatavyo:

"Ikiwa sio mtawala ndiye mwenye kuongoza Ijumaa na Idi, bali ni imamu aliyeteuliwa na nchi au kukawa hakuna imamu mwingine na huyu aliyewekwa ni Faasiq, kunaswali nyuma yake au hakuswaliwi? Jibu ni kwamba kunaswaliwa nyuma ya Faasiq katika hali mbili:

Endapo utaswali nyuma yake basi irudi swalah yako. Ikiwa imamu siku ya Ijumaa ni mtu Jahmiy na ndiye mtawala, swali nyuma yake na irudi swalah

---

Hali ya kwanza: Ikiwa huyu ndiye mtawala wa waislamu na watu hawana imamu mwingine isipokuwa huyu. Yule anayeswali peke yake na akaacha kuswali nyuma yake, Ahl-us-Sunnah wanaonelea kuwa ni mzushi.

Hali ya pili: Ikiwa tendo hilo halitopelekea katika uharibifu kwa kuacha kuswali nyuma yake. Kwa mfano kukatokea mizozo kati ya waislamu na fitina na chuki.

Ama kukiwa kuna imamu mwingine na hilo halipelekei katika uharibifu ukaswali nyuma yake na ukaacha kuswali nyuma ya imamu ambaye ni mwadilifu, hapa ndipo wanachuoni wametofautiana kama swalah inasihi au haisihi.

Hanaabilah na Maalikiyyah wanaonelea kuwa swalah si sahihi na ni wajibu kurudi kuiswali tena. Shaafi´iyyah na Ahnaaf wanaonelea kuwa swalah ni sahihi pamoja na kwamba imechukizwa. Hii ndio kauli sahihi. Sahihi ni kwamba swalah inasihi pamoja na machukizo. Dalili ya hili ni yale yaliyothibiti katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy kupitia Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Wawaswalisheni - yaani maimamu wenu - wakipatia, wana fungu lao na nyinyi mna fungu lenu, na wakikosea, mna fungu lenu na wao hawana kitu." al-Bukhaariy (694).

Hadiyth hii inaonesha wazi kuwa imamu akikosea kosa linampata yeye mwenyewe. Ama kuhusu maamuma hawapati kitu katika hilo.

Vilevile imethibiti kuwa Maswahabah walikuwa wakiswali nyuma ya Hajjaaj bin Yuusuf na alikuwa ni Faasiq na dhalimu. Kadhalika Maswahabah waliswali nyuma ya Waliyd bin ´Uqbah bin Abiy Mu´aytw ambaye alikuwa ni kiongozi wa Kuufah kabla ya ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh). Mtu huyu alikuwa ni Faasiq anakunywa pombe. Mpaka siku moja aliwaswalisha Fajr na alikuwa amelewa ambapo aliwaswalisha Rakaa nne kisha akawageukia na kuwauliza "Mnataka niwazidishie?" ´Abdullaah bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) akamwambia "Tangu tuko na wewe hujapatapo kuzidisha!" halafu akarudi kuswali tena na akaenda kumshtaki kwa kiongozi mkuu akampiga bakora na kumwondosha.

Imethibiti pia katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy kwamba ´Uthmaan bin ´Affaan (Radhiya Allaahu ´anh) watu wa mapinduzi walimtinga nyumbani kwake kutaka kumuua - watu hawa ni mafusaki - ilipofika wakati wa swalah akatangulia mbele mtu mmoja wa mapinduzi na kutaka kuwaongoza watu. Ndipo akaja mtu na kumuuliza kiongozi wa waumini ´Uthmaan kwa kumwambia: "Ee kiongozi wa Mtume wa Allaah! Muda wa swalah umefika sasa na kuna mtu mmoja katika watu wa mapinduzi anataka kutuongoza katika swalah. Je, tuswali nyuma yake ilihali ni Faasiq?" Akamwambia: "Ee ndugu yangu! Hakika ya swalah ni miongoni mwa vitu bora wanavyofanya watu! Akifanya vizuri nanyi fanyenyi vizuri pamoja naye na endapo ataharibu basi jiepusheni na kuharibu kwake." al-Bukhaariy (695).

Maandiko haya yanatolea dalili kuonesha kuwa kuswali nyuma ya mtu Faasiq ni sahihi na hairudiliwi. Lakini hata hivyo ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba lililo bora ni kuswali nyuma ya mtu ambaye ni mwadilifu." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (02/530-531)

[91] Mu´attwil, bi manaa ni yule mwenye kukanusha majina na sifa za Allaah.

yako. Lau imamu atakuwa ni mtawala, au mtu mwingine, na akawa ni mwenye kufuata Sunnah, swali nyuma yake na wala usiirudi swalah yako.

125- Kuamini kuwa Abu Bakr na ´Umar pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wako kwenye chumba cha ´Aaishah. Walizikwa pamoja naye. Ukiliendea kaburi, basi unatakiwa kuwasalimia baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

126- Ni wajibu kuamrisha mema na kukataza maovu, isipokuwa ambaye unachelea upanga au kiboko chake[92].

127- Inatakiwa kuwasalimia waja wa Allaah wote.

128- Ambaye anaacha swalah ya Ijumaa na ya mkusanyiko msikitini bila ya udhuru wowote, ni Mubtadi´. Miongoni mwa nyudhuru kunaingia pia maradhi yenye kumzuia mtu kutoweza kwenda msikitini au kumuogopa mtawala mwenye kudhulumu. Yasiyokuwa haya hayazingatiwi kuwa ni udhuru wowote.

129- Mwenye kuswali nyuma ya imamu na asimfuate, swalah yake si sahihi[93].

130- Kuamrisha mema na kukataza maovu kunakuwa kwa mkono, mdogo na moyo, bila ya upanga[94].

131- Muislamu aliyesitirika ni yule asiyedhihirisha mashaka yoyote.

---

[92] Kuna sharti tatu za kuamrisha mema na kukataza maovu. Imaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Elimu, upole na subira ni mambo ya lazima katika suala hili. Elimu kabl ya kuamrisha na kukataza, upole pindi uko unafanya hivo na subira baada yake." (Majmuu´-ul-Fataawaa (28/137))

[93] Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Imamu amewekwa ili afuatwe. Pindi anapokabiri, nanyi kabirini na msikabiri kabla ya yeye kukabiri, pindi anaposujudu, nanyi sujuduni na msisujudu kabla ya yeye kusujudu, anaposema "Sami´ah Allaahu liman hamidah", semeni "Rabbanaa Lak-al-Hamd", anaposwali kwa kusimama, nanyi swalini kwa kusimama na anaposwali kwa kukaa, nanyi swalini kwa kukaa." (Ahmad (02/230) na Abu Daawuud (306)). al-Albaaniy amesema: "Mlolongo wa wapokezi wake ni Swahiyh." (Irwaa´-ul-Ghaliyl (02/121))

[94] Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Yule katika nyinyi ambaye ataona maovu basi ayaondoshe kwa mkono wake. Ikiwa hawezi, ayaondoshe kwa ulimi wake. Ikiwa hawezi, [ayaondoshe] kwa moyo wake - na hiyo ni imani dhaifu kabisa." (Muslim (78))

132- Elimu yoyote ya ghaibu ambayo mja anatamka kwayo na si yenye kupatikana katika Qur-aan wala Sunnah, ni Bid´ah na upotevu. Haimpasi yeyote kuitendea kazi wala kulingania kwayo.

133- Mwanamke yoyote mwenye kujioza mwenyewe kwa mwanaume si halali kwake[95], isipokuwa kwa kuwepo walii, mashahidi wawili waadilifu pamoja na mahari. Katika hali nyinginezo wanatakiwa kuadhibiwa endapo watafanya kitu.

134- Ukimuona mtu anamtukana yoyote katika Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi elewa kuwa ni mtu mwenye maoni maovu na ni mtu mwenye kufuata matamanio yake. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Wanapotajwa Maswahabah zangu basi nyamazeni."

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alijua watayoteleza baada ya kufa kwake, lakini hakusema juu yao isipokuwa kheri. Amesema:

"Waacheni Maswahabah zangu na msisemi juu yao isipokuwa kheri tu."[96]

Usizungumze kitu juu ya kuteleza kwao, vita vyao wala yale ambayo elimu yake imefichikana kwako. Usimsikize yeyote anayeyazungumzia, hakika moyo wako hautasalimika endapo utasikiza kitu.

135- Ukimsikia mtu anayatukana au kuyarudisha mapokezi au anatamani kitu kingine mbali na mapokezi, basi utuhumu Uislamu wake na usishuku kuwa ni mtu mwenye kufuata matamanio na Mubtadi´.

---

[95] Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mwanamke hamuozeshi mwanamke mwenzie wala mwanamke hajiozeshi mwenyewe. Hakika mwanamke mwenye kujiozesha mwenyewe si jengine isipokuwa tu ni uzinifu." (Ibn Maajah (1882), ad-Daaraqutwniy (384) na al-Bayhaqiy (07/110))

Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ni Swahiyh isipokuwa sentesi ya mwisho... Abu Hurayrah amesema: "Mwanamke mwenye kujiozesha mwenyewe tulikuwa tukionelea kuwa ni mzinifu." Sentesi ya mwisho ni kutoka kwa Swahabah na imepokelewa na ad-Daaraqutwniy na al-Bayhaqiy. Ninasema: Mlolongo wa wapokezi wake ni Swahiyh kwa masharti ya al-Bukhaariy na Muslim." (Irwaa´-ul-Ghaliyl (1841))

[96] al-Bazzaar katika "Kashf-ul-Astaar" (03/290).

136- Tambua kuwa manyanyaso ya mtawala hayapunguzi zile faradhi alizoweka Allaah (´Azza wa Jall) kupitia kwa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Jukumu la ukandamizaji wake liko juu yake. Matendo yako na utiifu wako wa Sunnah ni mtimilifu - Allaah (Ta´ala) akitaka. Bi maana: swalah ya mkusanyiko, swalah ya ijuma na Jihaad inatakiwa kufanywa pamoja nao. Shirikiana naye katika aina zote za utiifu - uko pamoja na nia yako[97].

137- Ukimuona mtu anaomba du´aa dhidi ya mtawala, basi tambua kuwa ni mtu anayefuata matamanio. Ukimuona mtu anamuombea mtawala du´aa ya kutengemaa, basi tambua kuwa ni mtu wa Sunnah - Allaah akitaka. Fudhwayl bin ´Iyaadhw amesema:

"Lau mimi ningelikuwa na du´aa yenye kuitikiwa, basi nisingeijalia isipokuwa tu kwa mtawala."

Ahmad bin Kaamiyl amesema: "al-Husayn bin Muhammad at-Twabariy amesimulia, kutoka kwa as-Swaa-igh, ambaye amesema: "Nimemsikia Fudhwayl akisema:

"Lau mimi ningelikuwa na du´aa yenye kuitikiwa, basi nisingeijalia isipokuwa tu kwa mtawala." Kukasemwa: "Ee Abu ´Aliy! Tufafanulie hili!" Akasema: "Nikijiombea mwenyewe, itakuwa ni kwangu pekee. Nikimuombea mtawala na akanyooka, basi watanyooka vilevile waja na miji kupitia kutengemaa kwake."

Tumeamrishwa kuwaombea utengemavu na hatukuamrishwa kuomba dhidi yao, hata kama watadhulumu na kudhulumu. Hili ni kwa sababu ukandamizaji wao na dhulumu zao ni juu yao wenyewe, ilihali kutengemaa kwao ni juu yao wenyewe na kwa waislamu.

138- Usimtaje yeyote katika mama wa Waumini isipokuwa kwa kheri tu.

139- Ukimuona mtu anahifadhi swalah za faradhi na mkusanyiko pamoja na mtawala na wengineo, basi tambua kuwa ni mtu wa Sunnah - Allaah (Ta´ala)

---

[97] Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Haijuzu kumpiga vita mtawala kwa sababu tu ya dhambi, hata kama mtu aliyesimamishiwa adhabu ni lazima kuuawa kwa sababu ya baadhi ya madhambi, kama mfano wa zinaa. Kila ambacho ni lazima kuuawa kwacho, haina maana kwamba ni lazima kumpiga vita mtawala kwa kitendo hicho hicho, kwa sababu ufisadi wa vita ni mbaya zaidi kuliko ile dhambi kubwa alofanya mtawala." (Majmuu´-ul-Fataawaa (22/61))

akitaka. Na ukimuona mtu anapuuza swalah za faradhi na mkusanyiko, hata kama atakuwa na mtawala, basi tambua kuwa ni mtu wa matamanio.

140- Ya halali ni yale uliyoyashuhudia na ukaapa kwayo ya kwamba ni halali na hali kadhalika ya haramu. Yale yenye kutia shaka kifuani mwako hayo yana utata.

141- Msitiriwaji ni yule ambaye sitara yake imethibitishwa na mfedheheshwaji ni yule ambaye fedheha yake imethibitishwa.

142- Ukimsikia mtu anasema: "Fulani ni Mushabbih, fulani anatamka kwa Tashbiyh[98]", basi mtuhumu na ujue kuwa huyo ni Jahmiy. Ukimsikia mtu anasema: "Fulani ni Naaswibiy[99]", basi tambua kuwa huyo ni Raafidhwiy. Ukimsikia mtu anasema: "Zungumza kwa Tawhiyd! Nifafanulie Tawhiyd", elewa kuwa huyo ni Khaarijiy, Mu´taziliy[100]. Akisema: "Fulani ni mtenzwa nguvu " au anazungumza kwa Kutenzwa nguvu[101] au Uadilifu, basi tambua

---

[98] Imaam Ibn ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amefafanua neno "Tashbiyh" (kushabihisha) ifuatavyo:

"Ni kuthibitisha anayeshabihiana na Allaah katika haki au sifa ambazo ni maalum Kwake Pekee. Hii ni kufuru kwa sababu ni kumshirikisha Allaah. Vilevile ndani ya kitendo hicho kuna kumtukana Allaah kwa vile Amemshabihisha na viumbe wapungufu." (Sharh Lum´at-il-I´tiqaad, uk. 34)

[99] Wingi ni Nawaaswib. ´Allaamah ´Abdul-´Aziyz ar-Raajhiy (Hafidhwahu Allaah) amesema alipokuwa akielezea madhehebu ya Nawaaswib na Khawaarij:

"Madhehebu ya watu hawa ni kinyume na madhehebu ya Raafidhwah ambayo ni kuwachukia watu wa nyumba ya kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Ahl-ul-Bayt na kuwafanyia uadui.

Wameitwa Nawaaswib kwa kuwa wamejenga uadui kwa Ahl-ul-Bayt.

Wameitwa Khawaarij kwa sababu walimfanyia uasi ´Aliy na wakamfanyia al-Baraa´ baada ya masuala ya hukumu. Hali kadhalika wakamfanyia al-Baraa´ ´Uthmaan baada ya kuwajongeza ndugu zake kwa kuitakidi kwao kuwa amekuwa Faasiq kwa tendo hilo na amemuasi Allaah. Waliosalia katika Maswahabah hawawafanyii al-Baraa´ isipokuwa tu wale ambao wanaonelea kuwa wametenda dhambi kubwa kwa mtazamo wao." (al-Hidaayah ar-Rabbaaniyyah fiy Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah (02/750-751)

[100] Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Tawhiyd anayoikusudia mwandishi (Rahimahu Allaah) ni ya Mu´tazilah. Mu´tazilah wana misingi mitano ambapo mmoja wapo ni Tawhiyd. Wanachokusudia ni kukanusha sifa za Allaah (Tabaarak wa Ta´ala)." (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah (142))

[101] Ijbaar. Shaykh Swaali Aalush-Shaykh (Hafidhwahu Allaah) amesema kuhusu kundi hili la Jabriyyah yafuatayo:

"Jabriyyah wamegawanyika sehemu mbili:

kuwa huyo ni Qadariy, kwa sababu majina yote haya yamezushwa na watu wa matamanio.

143- ´Abdullaah bin al-Mubaarak amesema:

"Usichukue chochote kilicho na Rafdhw[102] kutoka al-Kuufah. Usichukue chochote kilicho na upanga kutoka kwa watu wa ash-Shaam. Usichukue chochote kilicho na Qadar[103] kutoka al-Basrah. Usichukue chochote kilicho na Irjaa´[104] kutoka Khuraasaan. Usichukue chochote kilicho na Swarf[105] kutoka Makkah. Usichukue chochote kilicho na nyimbo kutoka al-Madiynah. Usichukue chochote kutoka kwao kuhusiana na haya mambo.

144- Ukimuona mtu anampenda Abu Hurayrah, Anas bin Maalik, Usayd bin Hudhwayr, basi tambua kuwa ni mtu wa Sunnah - Allaah akitaka.

Ukimuona mtu anampenda Ayyuub, Ibn ´Awn, Yuunus bin ´Ubayd, ´Abdullaah bin Idriys al-Awdiy, ash-Sha´biy, Maalik bin Mighwal, Yaziyd bin Zuray´, Mu´aadh bin Mu´aadh, Wahb bin Jariyr, Hammaad bin Salamah, Hammaad bin Zayd, Maalik bin Anas, al-Awzaa´iy na Zaaidah bin Qudaamah, basi jua kuwa ni mtu wa Sunnah.

Ukimuona mtu anampenda Ahmad bin Hanbal, al-Hajjaaj bin Minhaal na Ahmad bin Naswr, akawataja kwa uzuri na akafuata maoni yao, basi tambua kuwa ni mtu wa Sunnah.

---

1- Jabriyyah waliopindukia: Hawa ni wale wanaosema kuwa mwanaadamu hana khiyari kabisa. Wanasema ni kama bendera yenye kuendeshwa na upepo. Hii ndio I´tiqaad ya Jahmiyyah na kundi katika Suufiyyah waliopundukia. Wanapatikana leo.

2- Jabriyyah ambao hawakupindukia: Hawa ni Ashaa´irah. Hakika Ashaa´irah wanazungumza kwa I´tiqaad ya Jabriyyah, lakini hata hivyo ni madhehebu ya Jabriyyah ya ndani na sio ya dhahiri. Wanasema kwamba udhahiri wa mja ni kwamba ni mwenye khiyari, lakini uhakika wa mambo ni kwamba ametenzwa nguvu kwa ndani. Kwa ajili hii ndio maana wakazua tamko la ´kuchuma`. Wamesema kuwa matendo ni chumo la mja. Nini maana yake? Viongozi wao wametofautiana juu ya kufasiri neno ´chumo` katika maoni kumi na moja. Hatuna nafasi ya kutaja maoni haya hapa. Lakini kwa ufupi wanachotaka ni kwamba hawaonelei kama kuna maana yoyote ya kuchuma/kutenda." (Sharh Lum´at-il-I´tiqaad, uk. 99-100)

[102] Madhehebu ya Raafidhwah.

[103] Madhehebu ya Qadariyyah.

[104] Madhehebu ya Murji-ah.

[105] Kuuza fedha kwa dhahabu na kinyume chake.

145- Ukimuona mtu anakaa na mtu kutoka katika watu wa matamanio, basi mtahadharishe na mzindue. Akiendelea kukaa nao baada ya kujua, jitenge mbali naye, kwani hakika huyo ni mtu wa matamanio[106].

146- Ukisikia mtu mwenye kuyasikia mapokezi na hali ya kuwa hayataki, badala yake anataka Qur-aan, hakuna shaka ya kwamba ni mtu aliye na uzandiki. Simama kutoka kwake na achana naye[107].

147- Tambua kuwa matamanio yote ni maovu. Yote yanaita kwenye upanga. Mabaya zaidi kati yao ni Raafidhwah, Mu´tazilah pamoja na Jahmiyyah, hakika wanachotaka ni kuwaongoza watu katika ukanushaji na uzandiki.

148- Tambua kuwa mwenye kumshambulia yoyote katika Maswahabah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), anachotaka ni kumshambulia Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na amemuudhi ndani ya kaburi lake.

149- Ukidhihirikiwa na kitu katika Bid´ah kutoka kwa mtu, tahadhari naye. Kwani hakika yale yaliyofichikana kwako ni mengi kuliko yale yaliyodhihiri.

150- Ukimuona mtu katika Ahl-us-Sunnah ambaye njia na mwenendo wake ni mbaya na ni mtenda dhambi, muovu, mtenda maasi na mpotevu na wakati huo huo yuko katika Sunnah, tangamana naye na kaa naye, hakika maasi yake hayatokudhuru. Ukimuona mtu ni mwenye kujitahidi katika ´ibaadah, mwenye kuipa kisogo dunia na mwenye bidii kweli katika ´ibaadah na wakati huo huo akawa ni mtu mwenye matamanio, usiikae naye, usiyasikilize maneno yake na wala usitembee naye kwenye barabara, kwani mimi nachelea

---

[106] Imaam Abu Daawuud as-Sijistaaniy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Nilisema kumwambia Abu ´Abdillaah Ahmad bin Hanbal: "Nikimuona mtu katika Ahl-us-Sunnah anakaa na Ahl-ul-Bid´ah, je niache kuzungumza naye?" Akasema: "Hapana. Mbainishie kuwa ambaye umemuona anakaa naye ni mtu wa Bid´ah. Akiachana naye endelea kuzungumza naye, lakini asipofanya hivo, basi mtazame kama huyo mwengine. Ibn Mas´uud amesema: "Mtu ni kama swahiba wake."" (Twabaqaat-ul-Haanaabilah (01/160) ya Imaam Ibn Abiy Ya´laa)

Kulisemwa kuambiwa Imaam al-Awzaa´iy (Rahimahu Allaah):

"Kuna mtu anasema: "Mimi nakaa pamoja na Ahl-us-Sunnah na Ahl-ul-Bid´ah."" Akasema: "Mtu huyu anachotaka ni kusawazisha haki na batili." (al-Ibaanah (02/456))

[107] Imaam Abu Qilaabah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ukizungumza na mtu juu ya Sunnah, halafu baadae akakujibu kwa kusema: "Achana na haya na badala yake tupe Kitabu cha Allaah", basi utambue kuwa ni mpotevu." (Siyaar A´laam-in-Nubalaa´ (04/472))

usije kuridhia njia yake na hatimaye ukawa ni mwenye kuangamia pamoja naye[108].

Yuunus bin ´Ubayd alimuona mwanawe akitoka kwa mtu wa matamanio akamwambia:

"Ee mwanangu, umetoka wapi?" Akasema: "Kutoka kwa fulani." Akamwambia: "Ee mwangu, napendelea zaidi kukuona unatoka kwenye nyumba ya huntha kuliko kukuona unatoka kwenye nyumba ya fulani na fulani. Ee mwanangu, napendelea zaidi ukutane na Allaah hali ya kuwa ni mzinifu, mtenda dhambi, mwizi na mfanya khiyana kuliko ukutane Naye na maoni ya fulani na fulani."[109]

Huoni kuwa Yuunus bin ´Ubayd alitambua kuwa huntha hawezi kumfanya mwanawe akapotea na dini yake, ilihali mtu wa Bid´ah anaweza kumpotosha mpaka akakufuru.

151- Tahadhari na khaswa khaswa na watu wa zama zako na tazama ni nani unakaa naye, ni nani unamsikiza na kusuhubiana naye, kwani ni kana kwamba viumbe wako katika kuritadi isipokuwa wale waliokingwa na Allaah.

152- Tazama ukimsikia mtu anamtaja Ibn Abiy Du-aad, Bishr al-Mirriysiy, Thumaamah, Abu Hudhayl, Hishaam al-Fuutwiy au yeyote katika wafuasi wao. Katika hali hiyo tahadhari naye, kwani hakika ni mtu wa Bid´ah. Watu hawa walikuwa katika kuritadi. Achana na mtu huyu ambaye anawasema vizuri na yule aliyemtaja katika wao.

153- Kuwatia wengine katika mtihani ni jambo la Bid´ah. Ama kuhusu leo, wanapewa mtihani kwa Sunnah, kutokana na maneno yake:

---

108 Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mtu kukutana na Allaah akiwa na aina zote za dhambi isipokuwa shirki, ni bora kuliko kukutana Naye akiwa na kitu katika matamanio." (al-I´tiqaad, uk. 158 ya al-Bayhaqiy)

109 Abu Nu´aym (03/20-21), al-Khatwiyb al-Baghdaadiy katika "Taariykh Baghdaad" (12/172-173) na wengineo.

"Hakika elimu hii ni dini. Hivyo basi, kuwa mwangalifu ni kutoka kwa nani mnaichukua dini yenu."[110]

Pia:

"Msiikubali Hadiyth isipokuwa kutoka kwa yule mnayekubali ushuhuda wake."[111]

Kwa hivyo unatakiwa kuangalia. Ikiwa mtu ni mtu wa Sunnah, mjuzi na ni mkweli, andika kutoka kwake. Vinginevyo achana naye.

154- Ukitaka kuwa na msimamo juu ya haki na kuwafuata waliokuwa kabla yako walioko katika njia ya Ahl-us-Sunnah, tahadhari na falsafa na wenye kujishughulisha na falsafa, mijalada, ubishi, kipimo na magomvi katika dini. Hakika kuwasikiliza kwako - hata kama hutokubali kitu kutoka kwao - kunapenyeza shaka ndani ya moyo. Kunatosheleza mtu akayakubali na akaangamia. Hakupatapo kamwe kuwepo uzandiki, Bid´ah, matamanio wala upotevu, isipokuwa ni kwa ajili ya falsafa, mijadala, ubishi na kipimo. Yote haya ndio mlango wa Bid´ah, mashaka na uzandiki.

155- Jikumbushe nafsi yako juu ya Allaah. Jilazimie mapokezi, watu wake na yafuate. Hakika dini ina maana ya kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) peke yake na Maswahabah zake. Waliokuwa kabla yetu hawakutuacha katika utatizi. Wafuate, ustarehe na usiyavuke mapokezi na watu wake.

156- Simama katika yenye kutatiza na wala usilinganishe kitu.

157- Usitafute hila ambazo kwazo ukafikiria kuwaraddi Ahl-ul-Bid´ah. Umeamrishwa kuwanyamazia na wala usiwape fursa juu ya nafsi yako. Hujui ya kwamba Muhammad bin Siyriyn - pamoja na fadhila zake - hakumjibu mtu

---

110 Ibn ´Adiy katika "al-Kaamil" (01/155), as-Sahmiy katika "Taariyk Jarjaan", uk. 473 na Ibn-ul-Jawziy katika "al-Waahiyaat" (01/131). Shaykh Khaalid ar-Raddaadiy (Hafidhwahu Allaah) amesema:

"Mnyororo ni dhaifu sana kwa sababu ya Khaalid bin Du´luj ambaye ni dhaifu mno, kama ilivyotajwa katika "al-Miyzaan" (01/352-353)." Lakini hata hivyo maneno haya yamesihi kutoka kwa Imaam Muhammad bin Siyriyn (Rahimahu Allaah) na yanapatikana kwa Muslim (01/31), "al-Kaamiyl" (01/155) ya Ibn ´Adiys, Abu Nu´aym (02/278) na wengineo. (Taaliki ya Sharh-us-Sunnah" (153))

111 ar-Raamharmaziy katika "al-Muhaddith al-Faaswil", uk. 41, Ibn ´Adiy katika "al-Kaamil" (01/159) na al-Khatwiyb al-Baghdaadiy katika "al-Kifaayah", uk. 125-126. Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema kuwa ni yenye kuzushwa katika "Dhwa´iyf al-Jaami´" (6193).

kutoka katika Ahl-ul-Bid´ah katika suala moja tu? Hakukubali kusikia Aayah japo moja kutoka katika Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jall). Alipoulizwa juu ya hilo akasema:

"Ninachelea asije kuipotosha na hivyo kukaingia kitu ndani ya moyo wangu."[112]

158- Ukimsikia mtu anasema: "Hakika sisi tunamuadhimisha Allaah", pindi anaposikia mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi tambua kuwa huyo ni Jahmiy. Anachotaka ni kuyarudisha mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kuyatupilia mbali kwa maneno haya. Anadai kuwa anamuadhimisha Allaah na kumtakasa pale anaposikia Hadiyth kuhusu Kuonekana kwa Allaah Aakhirah, Kushuka kwa Allaah na mfano wazo. Je, mtu huyu hayarudishi mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Akisema: "Hakika sisi tunamuadhimisha Allaah kutoka sehemu kwenda nyingine", amedai kuwa yeye ni mjuzi zaidi juu ya Allaah kuliko wengine. Tahadhari na watu hawa, hakika wengi katika watu wasio wasomi - vilevile na wengineo - wako katika hali kama hii. Tahadharisha watu nao!

159- Akiwepo mtu anayetaka kuongoka atakuuliza kitu kilichomo ndani ya kitabu hiki, basi zungumza naye na mwongoze. Hata hivyo endapo atakuja kutaka kujadiliana nawe, tahadhari naye. Hakika katika mijadala kuna ubishi, ushindani, ugomvi na kukasirika. Hakika wewe umekatazwa sana yote haya. Haya yanamtoa mtu katika njia ya haki. Hatukupata khabari ya yeyote katika Fuqahaa´ wala wanachuoni wetu ya kwamba alijadiliana, kubishana au kugombana. al-Hasan al-Baswriy amesema:

"Mwenye hekima habishani na wala hashindani. Hekima yake ni kuieneza. Ikikubaliwa basi anamhimidi Allaah na ikirudishwa anamhimidi Allaah."[113]

Kuna mtu alikuja kwa al-Hasan akamwambia: "Nataka kujadiliana na wewe katika dini!" al-Hasan akasema:

"Kuhusu mimi, naielewa dini yangu. Lakini kama dini yako imepotea, nenda ukaitafute."[114]

---

[112] ad-Daarimiy (01/91), Ibn Wadhdhwaah katika "al-Bid´ah", uk. 53 na wengineo.

[113] al-Ibaanah al-Kubraa (661) ya Ibn Battwah na wengineo.

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwasikia watu waliokuwa wamesimama nje ya chumba chake wakijadiliana. Mmoja wao anasema: "Je, Allaah hakusema kadhaa?" Mwengine naye akijibu: "Je, Allaah hakusema kadhaa?" Akatoka hali ya kukasirika na kusema:

"Je, haya ndio mliyoamrishwa? Nilitumwa kwenu kwa haya? Mnafanya sehemu ya Kitabu cha Allaah kugonga nyingine?"

Hivyo akakataza mijadala.

Ibn ´Umar alikuwa akichukia mijadala na hali kadhalika Maalik bin Anas na waliokuwa juu yao na waliokuwa chini yao, mpaka hii leo. Maneno ya Allaah (´Azza wa Jall) ni makubwa kuliko maneno ya viumbe. Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) amesema:

مَا يُجَادِلُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا

"Habishani katika *Aayaat* za Allaah isipokuwa wale waliokufuru."[115]

Kuna mtu alimuuliza ´Umar bin al-Khattwaab: "Ni nini:

وَالنَّاشِطَاتِ نَشْطًا

"Wanaotoa kwa upole."[116]

Akamjibu:

"Lau ungelikuwa umenyoa kipara, basi ningekata shingo yako."[117]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Muumini habishani. Sintomshufaia mwenye kubishana siku ya Qiyaamah. Acheni ubishi, kutokana na uchache wa kheri yake."[118]

---

[114] Tazama maelezo nambari 10.

[115] 40:04

[116] 79:02

[117] ad-Daarimiy (01/51) na wengineo.

[118] at-Twabaraaniy katika "al-Kabiyr" (08/178-179), Ibn Battwah katika "al-Ibaanah al-Kubraa" (02/489-490) na wengineo. Imaam al-Haythamiy (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu mlolongo wa Hadiyth: "Kumekuja Kathiyr na ni mtu dhaifu sana." (Majma´-uz-Zawaa-id (01/156) na (07/259). Kadhalika

160- Haijuzu kwa Muislamu kusema: "Fulani ni mtu wa Sunnah, mpaka atambue kuwa amekusanya vipengele vyote vya Sunnah. Hakusemwi juu yake "Mtu wa Sunnah" mpaka akusanye Sunnah yote.

161- ´Abdullaah bin al-Mubaarak amesema:

"Asli ya matamanio sabini na mbili ni matamanio mane. Kutoka katika matamanio haya mane ndio kumechipuka matamanio haya sabini na mbili: Qadariyyah, Murji-ah[119], Shiy´ah na Khawaarij."[120]

Yule mwenye kuonelea kuwa Abu Bakr, kisha ´Umar, kisha ´Uthmaan na halafu ´Aliy wanakuja mbele ya Maswahabah wengine wote wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), asiwazungumzie wengine isipokuwa kwa kheri tupu na akawaombea du´aa, ameiacha Tashayyu´[121] kuanzia mwanzo hadi mwisho wake.

Mwenye kusema kuwa imani ni (kuamini), maneno na vitendo na kwamba inazidi na kupungua, ameiacha Irjaa´ yote kuanzia mwanzo hadi mwisho wake.

Mwenye kusema kuwa kunaswaliwa nyuma ya kila mwema na mwovu[122], Jihaad itaendelea pamoja na kila mtawala[123], asionelei kufanya uasi dhidi ya

---

amesema: "Kumekuja Kathiyr bin Marwaan. Yahyaa na ad-Daaraqutwniy wamesema kuwa ni mwongo." (Majma´-uz-Zawaa-id (01/106))

119 Imaam Sufyaan ath-Thawriy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Tunatofautiana na Murji-ah kwa mambo matatu: Tunasema kuwa Iymaan ni (kuamini), kutamka na matendo, ilihali wao wanasema: "Kuamini na) kutamka pasi na matendo." Tunasema kuwa inazidi na kupungua, ilihali wao wanasema kuwa haizidi na wala haipungui. Tunasema kuwa Waislamu ni waumini vile tunavyojua, ama mbele ya Allaah, Allaah ndiye anajua zaidi. Wanasema: "Na sisi pia ni waumini mbele ya Allaah"." (Kitaab-ul-I´tiqaad wal-Hidaayah ilaa Sabiyl-ir-Rashaad, uk. 120-121 cha al-Bayhaqiy)

120 al-Ibaanah al-Kubraa (278) ya Ibn Battwah.

121 Madhehebu ya Shiy´ah.

122 Imaam Ibn ´Abdil-´Izz al-Hanafiy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Imethibiti katika "Swahiyh al-Bukhaariy" ya kwamba ´Abdullaah bin ´Umar na Anas bin Maalik waliswali nyuma ya al-Hajjaaj bin Yuuusuf ath-Thaqafiy ambaye alikuwa ni mtenda dhambi na mwenye kudhulumu." (Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah, uk. 374)

123 Imaam Ibn Qudaamah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Tunaonelea Hajj na Jihaad inafanywa na viongozi wote, sawa akiwa ni mwema au muovu. Hali kadhalika inajuzu kuswali Swalah ya Ijumaa nyuma yao."

mtawala kwa panga na akawaombea utengemavu, ameiacha ´Aqiydah ya Khawaarij kuanzia mwanzo hadi mwisho wake.

Mwenye kusema kuwa makadirio yote kheri na shari yake yanatokamana na Allaah (´Azza wa Jall), anampoteza na kumhidi Amtakaye, ameiacha ´Aqiydah ya Qadariyyah kuanzia mwanzo hadi mwisho wake na huyo ni mtu wa Sunnah.

162- Bid´ah zote zilizodhihiri ni kumkufuru Allaah Mtukufu. Mwenye kuzungumza kwazo ni kafiri bila ya shaka. Ambaye anaamini Kureja na kusema kwamba ´Aliy bin Abiy Twaalib yuhai na atarejea kabla ya siku ya Qiyaamah na hali kadhalika Muhammad bin ´Aliy, Ja´far bin Muhammad na Muusa bin Ja´far, akaongea juu ya uongozi na kwamba wao wanajua mambo yaliyofichikana na wamekingwa na kukosea, tahadhari naye, kwani hakika hawa na walio na maoni haya hawaamini Allaah Mtukufu.

163- Twa´mah bin ´Amr na Sufyaan bin ´Uyaynah wamesema:

"Anayesimama kwa ´Uthmaan na ´Aliy ni Shiy´iy[124]. Asiaminiwe, asizungumzishwe na wala mtu asikae naye. Mwenye kumtanguliza ´Aliy juu ya ´Uthmaan ni Raafidhwiy. Ameyakataa mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kuwatanguliza hawa watatu juu ya wengine na akawatakia rahmah waliobaki na akakomeka juu ya makosa yao, yuko katika njia iliyonyooka na uongofu juu ya suala hili."

---

Shaykh Swaalih Aalus-Shaykh (Hafidhwahu Allaah) amesema alipokuwa akiyashereheshа maneno haya:

"Miongoni mwa sifa za Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni kwamba wanaonelea kuhiji na kupigana Jihaad litaendelea kuwepo pamoja na viongozi wa waislamu. Ni mamoja wakawa ni wema au waovu. Inahusiana na maimamu ambao:

a) Uongozi wao umepita kwa kuteuliwa na Ahl-ul-Hall wal-´Aqd.

b) Uongozi wao umepita kwa kutumia mabavu.

Uongozi wote huu unahesabika ni wa Kishari´ah. Wana haki ya kutiiwa katika mema na kupigana Jihaad nyuma yao na kutowaasi. Kuwatii wao ni kumtii Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuwafanyia uasi au kutoamini kwamba ni wajibu kuwatii ni I´tiqaad ya Khawaarj na Mu´tazilah." (Sharh Lum´at-il-I´tiqaad, 149)

[124] Uchache wa Shiy´ah.

164- Sunnah ni kushuhudia ya kwamba wale Kumi ambao Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alishuhudia ya kuwa wako Peponi, wako Peponi pasi na shaka.

165- Usipambanue kumtumia salam zako isipokuwa tu juu ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na familia yake.

166- Tambua kuwa ´Uthmaan bin ´Affaan aliuawa hali ya kudhulumiwa na aliyemuua alikuwa ni mdhulumaji.

167- Mwenye kukubaliana na kitabu hichi, akakiamini na akakifanya kuwa ni kiigizo chema na wala asitilie shaka na kukanusha herufi yake hata moja, ni mtu wa Sunnah na Jamaa´ah. Ni mkamilifu, kwa sababu Sunnah imekamilika kwake. Ambaye atakanusha au kutilia shaka herufi moja ya kitabu hichi au akajitenga ni mtu wa matamanio.

168- Atayekanusha au akatilia shaka herufi moja ya Qur-aan au kitu kimechotoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), atakutana na Allaah hali ya kuwa ni mkadhibishaji. Mche Allaah na utahadhari na ichunge imani yako.

169- Ni katika Sunnah kutomsaidia yoyote katika kumuasi Allaah, si wale wema wala mwengine katika viumbe. Hakuna utiifu kwa kiumbe katika kumuasi Allaah. Asipendwe yeyote kwa hilo. Badala yake mtu anatakiwa kuchukia yote hayo kwa ajili ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

170- Kuamini kuwa tawbah ni lazima kwa waja na watubie kwa Allaah (´Azza wa Jall) kwa dhambi ndogo na kubwa.

171- Asiyemshuhudilia Pepo yule aliyeshuhudiliwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), huyo ni mtu wa Bid´ah na upotevu na ni mwenye kutilia shaka yale aliyosema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

172- Maalik bin Anas amesema:

"Ambaye atashikamana na Sunnah na wakasalimika naye Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kisha akafa, atakuwa pamoja na Mitume, wakweli, mashahidi na waja wema, hata kama atakuwa na matendo machache."

Bishr bin al-Haarith amesema:

"Uislamu ni Sunnah na Sunnah ni Uislamu."

Fudhwayl bin ´Iyaadhw amesema:

"Pindi ninapomuona mtu katika Ahl-us-Sunnah, nahisi ni kama kwamba nimemuona mmoja katika Maswahabah wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Pindi ninapomuona mtu katika Ahl-ul-Bid´ah, nahisi ni kama kwamba nimemuona mmoja katika wanafiki."

Yuunus bin ´Ubayd amesema:

"Ajabu ni kwa yule ambaye leo analingania katika Sunnah. Ajabu zaidi ni kwa yule anayeitikia na kuikubali Sunnah."[125]

Ibn ´Awn alikuwa akisema wakati wa kukata roho:

"Ala ala Sunnah! Ala ala Sunnah! Na tahadharini na Bid´ah." mpaka akakata roho.

Ahmad bin Hanbal amesema:

"Mmoja katika wenzangu alifariki na akaonekana ndotoni akisema: "Mwambieni Abu ´Abdillaah: "Jilazimie na Sunnah!", kwani hakika cha kwanza alichoniuliza Allaah ni juu ya Sunnah.""

Abul-´Aaliyah amesema:

"Mwenye kufa na kusitiriwa na Sunnah, huyo ni mkweli. Kunasemwa: "Kushikamana na Sunnah ni kuokoka.""

Sufyaan ath-Thawriy amesema:

"Mwenye kumsikiliza mtu wa Bid´ah, basi ametoka katika ulinzi wa Allaah na ametegemezwa mwenyewe kwayo - bi maana kwa Bid´ah."

Abu Daawuud bin Abiy Hind amesema:

"Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) alimfunulia Muusa bin ´Imraan: "Usikae na Ahl-ul-Bid´ah. Ukikaa nao na kukapenyeza ndani ya moyo wako kitu katika yale wanayoyasema, Nitakutupa Motoni.""[126]

---

[125] Abu Nu´aym (03/21), Ibn Battwah katika "al-Ibaanah al-Kubraa" (20) na wengineo.

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Mwenye kukaa na mtu wa Bid´ah basi hakupewa hekima."[127]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Usikae na mtu wa Bid´ah, kwani hakika mimi nachelea usije shukiwa na laana."[128]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Mwenye kumpenda mtu wa Bid´ah, basi Allaah atayaharibu matendo yake na ataiondosha nuru ya Uislamu katika moyo wake."[129]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Chukua njia nyingine kuliko ile anayopita mtu ambaye anakaa na mtu wa Bid´ah."[130]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Ambaye atamuadhimisha mtu wa Bid´ah, basi amesaidia kuubomoa Uislamu. Yule mwenye kumfanyia tabasamu Mubtadi´, ameyadharau yale Allaah (´Azza wa Jall) aliyomteremshia Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwenye kumuozesha binti yake Mubtadi´, basi amekikata kizazi chake. Mwenye kuliandama jeneza la Mubtadi´, hatoacha kuwa katika hasira za Allaah mpaka arejee."[131]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

---

126 Ibn Wadhdhwaah katika "al-Bid´ah", uk. 49.

127 al-Laalakaa´iy katika "as-Sunnah" (263) na (1149), Ibn Battwah katika "al-Ibaanah al-Kubraa" (439) na wengineo.

128 al-Laalakaa´iy (262) na Ibn Battwah (441) na (451).

129 al-Laalakaa´iy (263) na Ibn Battwah (440), Abu Nu´aym (08/103) na wengineo.

130 Abu Nu´aym (08/103), Ibn Battwah (493) na wengineo.

131 Abu Nu´aym (08/103).

"Nala na myahudi na mnaswara kuliko kula na Mubtadi´. Natamani kuwepo kati yangu mimi na mtu wa Bid´ah pazia ya chuma."[132]

Fudhwayl bin ´Iyadhw amesema:

"Allaah akijua kutoka kwa mtu kuwa anamchukia mtu wa Bid´ah, anamsamehe hata kama matendo yake yatakuwa machache. Mtu wa Sunnah hawezi kumsaidia mtu wa Bid´ah isipokuwa tu kwa unafiki. Ambaye atamgeuzia mgongo wake mtu wa Bid´ah, basi Allaah ataujaza moyo wake imani. Atakayemraddi mtu wa Bid´ah, basi Allaah atampa amani siku ya Khofu kubwa. Atayemtweza mtu wa Bid´ah, Allaah atamnyanyua Peponi kwa daraja mia moja - hivyo basi kwa ajili ya Allaah kamwe usiwe mtu wa Bid´ah!"

132 al-Laalakaa´iy (1149), Abu Nu´aym (08/103) na wengineo.